
**Waziri** aonya wanaorudisha wanafunzi kisa michango shule
UKURASA 5

**Mvua** yasababisha maafa, kaya 3,000 zazingirwa na maji
UKURASA 5

**Othmani** alia utovu maadili kwa watumishi
UKURASA 8




**Zinchenko: Ninaweza kwenda vitani Ukraine**
UKURASA 21

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 7, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581639
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Msuya ashtukia jambo wanaomzunguka Samia

• **Amsifu** kwa kasi miradi ya maendeleo, amtaka... *ukurasa 2*



Waziri Mkuu Mstaafu, Cleopa Msuya, akizungumza na waandishi wa habari (hawako pichani) nyumbani kwake jijini Dar es Salaam jana, wakati akieleza kuhusu umuhimu wa kudumisha Muungano wa Tanzania. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### TANAPA YANG'ARA TUZO ZA UMAHIRI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kupitia Idara ya Mawasiliano limeibuka mshindi katika tuzo za Umahiri katika Mawasiliano ya Umma zilizotolewa juzi mkoani Dar es Salaam...


UKURASA WA 17

### GUTERRES AONYA ISRAEL KUTUMIA AKILI BANDIA

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, amesema ana wasiwasi kuhusu taarifa ya uchunguzi inayoonyesha jeshi la Israel, linatumia akili bandia kutekeleza mashambulizi yake katika Ukanda wa Gaza...

## Mbunge ashangazwa kasi mikopo kausha damu, matumizi ya shisha

UKURASA 3



KUMBUKIZI MIAKA 52

UKURASA 4

## Karume bado anaishi kwa fikra, matendo na falsafa

**MICHEZO** YANGA YAMSHTAKI RASMI MWAMUZI CAF UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Msuya ashtukia jambo wanaomzunguka Samia

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, Cleopa Msuya, amesifu utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati, huku akimtahadharisha kuhusu watu wanaomzunguka kuwa wanaweza kuwa kikwazo kwake katika uchaguzi mkuu ujao.

Ameshauri serikali kuongeza nguvu katika kutangaza faida za Muungano ili kila mmoja aone haja ya kujivunia miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania.

Msuya pia amefafanua kauli aliyowahi kuitoa katika Bunge la Bajeti mwaka 1989 kuwa "kila mtu abebe msalaba wake", iliyopokewa kwa hisia tofauti na Watanzania.

Msuya alifunguka hayo jana katika mahojiano maalumu na waandishi wa habari yaliyofanyika nyumbani kwake, Upanga, Dar es Salaam, kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano ulioasisiwa Aprili 26, 1964 na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Abeid Aman Karume wa Zanzibar.

"Nilipata kuonana naye (Rais Samia) siku moja nikamwambia mama, tatizo lako katika uchaguzi ujao halitakuwa huko chini, labda tatizo litakuwa kwa hao watu wanaokuzunguka. Maana jina likipita CCM, kule chini watakupitisha tu.

"Kwa hiyo, mtazamo wangu ni kwamba anaendesha nchi kwa nia nzuri na amejitahidi kufanya watu wamuelewe na kwamba dalili zinaonyesha kuwa mambo yatakwenda sawa," alisema Msuya.

Pia alisema Rais Samia anaendesha mambo kwa nia nzuri na kwamba Tanzania inajivunia licha ya kasoro ndogo ambazo zimejitokeza katikati. Alisema Tanzania ni nchi ambayo inatawaliwa kisheria na katiba inaheshimika.

"Watu wote wa nje na wa ndani wanakubali hilo. Kila mmoja anafahamu namna alivyopatikana kuwa Rais. Mzee (Ali Hassan) Mwinyi alivyochaguliwa kuwa Rais lakini hivi karibuni baada ya kifo cha (Hayati John) Magufuli, automatically (moja kwa moja) Makamu wa Rais ambaye alikuwa Mama Samia akachukua mamlaka bila mtikisiko wowote.

"Ingekuwa nchi zingine ni vita na hasa kama ni mama lakini taratibu zikafuatwa akaapishwa kuwa Rais na yeye akamchagua Makamu wa Rais," alisema huku akibainisha kuwa ana matumaini makubwa naye kwa kuwa kuna vitu fulani amefanikiwa kuvifanya.



Waziri Mkuu Mstaafu, Cleopa Msuya, akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake jijini Dar es Salaam jana kuhusu umuhimu wa kudumisha Muungano wa Tanzania. **PICHA: JUMANNE JUMA**

"Alipochukua kapu (kuingia madarakani) kuna kauli mbili alizitoa. Ya kwanza, alisema, "Mnayemuona hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano si mama", kwa maneno mengine Rais ni institution (taasisi) ambayo alikuwa nayo, ni zilizile walizokuwa nazo wengine wote waliomtangulia," alisema.

Msuya alisema kauli hiyo imebeba ujumbe kuwa Rais ni taasisi na mamlaka aliyonayo ndiyo waliyokuwa nayo viongozi wengine waliopita.

Pia alisema alitoa kauli hiyo ili watu wajue kwamba hakuna mtu legelege pale juu na kwa upande mwingine, alionyesha alikuwa tayari kumaliza miradi ya kimkakati waliyoanza na mtangulizi wake.

"Kauli nyingine ambayo Rais Samia aliwahi kuitoa ni kuhusu yale aliyoanza na mwenzake (Rais Magufuli) miradi ya kimkakati atajitahidi aiendeleze na kuongeza mingine kila atakapoona inafaa," alisema Msuya.

### MTAZAMO SERIKALINI

Msuya alipongeza awamu zote sita za uongozi akisema kwa asilimia kubwa walioshika uongozi wamepambana kuhakikisha wanalinda Katiba na maslahi ya wananchi.

"Miongoni wa vitu ambavyo Watanzania wangejivunia ni kwamba pamoja na changamoto ambazo zimejitokeza hapa na pale, nchi inatawaliwa kwa misingi ya kisheria na Katiba yetu inaheshimika. Mtu yeyote wa ndani na nje anakubaliana na hilo.

"Kwa mfano, Mzee Mwinyi alipochaguliwa kuwa Rais baada ya Nyerere na hata hivi karibuni baada ya kifo cha Rais Magufuli, Rais Samia alichukua nafasi bila mtikisiko wowote tofauti na nchi zingine ambapo kungeweza kushuhudiwa vita," aliongeza.

Licha ya Katiba kuheshimu utaratibu uliotumika kumweka madarakani Rais Samia, alisema aliheshimu katiba katika kuteua Makamu wa Rais.

Kuhusu uongozi wa Rais Samia, alisema kwa asilimia kubwa umekuwa wa mafanikio na ameonyesha ujasiri mkubwa wa kuendeleza pale alipoishia mtangulizi wake.

### MUUNGANO

Msuya alitaka wananchi wauchukulie Muungano kwa mtizamo chanya badala ya kuleta hoja zisizo za msingi. Alisema Muungano ni kama ndoto yoyote, hazikosi changamoto na lazima yatafutwe majibu ya kukabiliana nazo.

"Muungano ni kitu kizuri. Unapoanza safari, kunakuwa na matatizo.

Ni muda mwafaka wananchi wajivunie kurithi Muungano ambao wengine wameshindwa kuuendeleza.

"Maana ya kuungana ni kupunguza gharama na kuongeza ufanisi. Maneno, changamoto zipo. Picha kubwa ni kwamba mafanikio yapo kwa sababu ya kuheshimu misingi ya mfumo," alisema.

Kwa mujibu wa Msuya, asilimia kubwa ya watu wanaobeza kuwapo kwa Muungano hata watapoulizwa matunda wanayoyaona kwa upande wa Bara watatoa jibu hilohilo.

"Serikali iweke juhudi za kuhakikisha wanaelimisha vijana kwa mbinu mbalimbali ili waweze kuelewa tija ya Muungano," alishauri.

### KAULI YAKE BUNGENI

Msuya alitoa ufafanuzi kuhusu kauli aliyowahi kuitoa katika Bunge la Bajeti la mwaka 1989 kuwa "Kila mtu abebe msalaba wake" ambayo ilipokewa kwa hisia tofauti na Watanzania.

"Hilo la kusema kwamba kila mtu abebe msalaba wake, ndio nilisema. Sababu yake ni nini? Tumepeleka bajeti hapo bungeni. Shida zetu ni zile zile ambazo mpaka leo Waziri wa Fedha anazikabili.

Mapato ya serikali ni madogo. Kwa hiyo katika bajeti ile tulibandikiza kodi katika kanga, vitenge na mambo mengine.

"Sasa katika hoja zilizotolewa pale ndani na wabunge, wengine walipinga hilo. Basi ooh! Mimi ninawake wawili nitawezaje kuvisha wake zangu wote wawili kanga na vitenge kama umepandisha kodi. Kwa kweli nikasema ni unafair (siyo sawa) kupandisha kodi taifa kwa kuwa umeona kuwa na luxury (anasa) ya kuwa na wake watatu.

"Niseme basi tutakuachia ili wanunulie kanga na vitenge wewe usiguswe. Lakini mimi nilie na mke mmoja niguswe. Kwa hiyo nilijibu hivyo," alisema na kubainisha kuwa kutokana na kauli hiyo, baadhi ya watu waliichukia na kusema hafai kuwa waziri na kwamba mbona si mjamaa.

"Kwa nini hataki kutoa vitu sawasawa kwa kila mtu akifikiri kwamba hiyo itaongeza kasi kwa huyo anayeteua mawaziri aamue kuniondoa au kutoniondoa. Mimi nilikuwa huru kabisa katika fikra zangu.

"Lakini bahati nilipokutana na Rais, ninafikiri siku mbili baadaye. Wakati ule alikuwa Mzee Mwinyi akaniambia bwana huku serikalini kuna kautaratibu una ripoti za siri zinaandikwa na idara ya usalama ambayo kila siku inakwenda kwa Rais.

"Inakwenda kwa Waziri Mkuu, ninafikiri kwa sasa hivi inaenda kwa Makamu wa Rais. Ilipofika kwake, alisema watu wenye baa kwenye mabasi wanasema, 'eeh, bwana! Afadhali tumeambiwa ukweli!

"Watu wanatudanganya tu. Huyu katuambia ukweli, kama unataka kuoa, nguvu yako, lakini usiwe mzigo kwa wenzako. Kwa hiyo wakajifuta wenyewe. "Unajua katika haya mambo ya politics (siasa) ukijaribu kutegemea sana umaarufu na siasa, Watanzania ni watu ambao wanafikiri mambo.

"Mimi nilisema vile kwa nia nzuri lakini mwitikio wake kwenye hizo ripoti zikasema majibu kwa watu wa kawaida kwenye mabasi, kwenye mabaa, kokote huko wanasema afadhali tumeambiwa ukweli bwana! "Hawa wengine wanatudanganya tu. Sasa mnaweza kuamua wenyewe kama ndiyo hiyo ilinifanya nikabaki pale. Nilikaa hazina kama mara mbili au mara tatu," alisema.

**IMEANDALIWA na Thobias Mwanakatwe, Mary Kadoke na Carlos Banda.**

HABARI KITAIFA

# Mbunge ashtushwa kasi ya shisha, mikopo 'kausha damu'

**Na Vitus Audax**, DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Cecilia Paresso (pichani), ameelezea kushtushwa na kasi ya matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo shisha pamoja na mikopo inayolalamikiwa, maarufu kama 'kausha damu' na kuitaka serikali kutilia mkazo sheria ili kunusuru jamii.



Akichangia juzi wakati wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/25, Paresso alisema ili taifa kuwa na maendeleo, lazima kuwapo ustawi wa jamii, watu kuwa na hali nzuri ya kiakili, kiafya na kiuchumi.

Paresso alisema kwa sasa matumizi ya shisha yamekuwa makubwa kupindukia, hususani kwa vijana wadogo ambao wanarundikana katika kumbi za starehe wakitumia kileo hicho, hali inayotengeneza wagonjwa watarajiwa wa baadaye.

"Nimesikia kwa Afrika Mashariki ni Tanzania tu bado tunatumia 'shisha', kwingine wamepiga marufuku. Je, sisi tunafanya nini katika hilo? Zaidi ya hapo, tunajiandaa kuja kuweka fedha nyingi katika sekta ya afya ili kuanza kutibu mzigo mkubwa wa wagonjwa wanaotokana na madhara hayo,"alisema

Alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kugharimia matibabu ya magonjwa makubwa yasiyoambukizwa ambayo yanasababishwa na mienendo mibovu ya watu, wakiwamo vijana wanaotumia shisha na kuwa magonjwa hayo yamekuwa yakitajwa kuongoza kwa kusababisha vifo Tanzania.

"Kila mara tumekuwa tukielezwa kuhusu madhara ya utumiaji wa vitu hivi hatari lakini tunafanyaje ili kuhakikisha tunadhibiti kabla havijaleta matatizo? Yawezekana ni biashara ya watu, lakini ni kwa kiwango gani na elimu inatolewa kwa kiwango gani ili mtu ajue?" alihoji.

Aliishauri serikali kuweka mkakati wa kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kudhibiti ongezeko la wakopeshaji wasiyokuwa rasmi maarufu 'kausha damu', ambao wamekuwa wakisababisha wananchi kufilisika.

"Iko mifuko ya kuwezesha wananchi kiuchumi zaidi ya 18, tuone namna ya kuiunganish pamoja na ile mikopo inayotolewa na halmashauri na kupata mfuko mmoja au miwili itakayoratibiwa na serikali na kutoa elimu kwa kuwafikia wananchi wa chini.

"Tuone ni namna gani tunaweza kuwasaidia kwa kuwakopesha kwa masharti nafuu na kuwanusuru na mikopo hiyo hatari, kwani wananchi hao wamekuwa wakishindwa kuzifikia benki kutokana na kuwapo kwa mashariti makubwa,"alisema.

Alisema kuna taasisi zinazotoa mikopo kisheria na kuonyesha shaka kwa baadhi kutosajiliwa na kutoa mikopo yenye athari katika jamii hadi kupewa majina tofauti kutokana na kusababisha madhira kwa wakopaji.

Mikopo hiyo, alisema huwa na riba kubwa na wakati mwingine imekuwa ikisambaratisha familia, matukio ya watu kujiua, huku wengine wakiua ndugu zao ili kupata fedha za kurejesha.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika hotuba yake kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya yake kwa mwaka 2024/25, alikiri kuwa vijana wenye umri wa miaka 30 na kuendelea wamebainika kuwa na magonjwa sugu.

Aliyataja magonjwa hayo ni pamoja na shinikizo la damu, kisukari pamoja na uzito uliozidi, licha ya elimu ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kutolewa kwa zaidi ya watu 1,107 nchini.

Kuhusu ustawi wa wananchi, Majaliwa alisema serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2023/24, kupitia programu hiyo, serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023.

Pia alisema wanakamilisha programu mbalimbali za kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kwa lengo la kuongeza fursa za kiuchumi na kuwajengea uwezo wa mbinu za kibiashara, kupata mitaji, masoko na mikopo.

Kadhalika, alisema imeanzisha madirisha maalum ya kuwezesha wanawake kupata mikopo yenye riba nafuu ili kupunguza umaskini kwa wanawake kwa kuwawezesha kupata mitaji.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2023/24, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, jumla ya mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.27 ilitolewa kwa miradi 56 ya vijana.

Utafiti uliofanywa na Dk. Anna Merchetti, kutoka nchini Uswizi na kupitishwa na katika jarida la afya la 'European Journal of Case Reports in Medicine' mwaka 2020, umebaini matumizi ya shisha kuwa chanzo cha ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) unaoshambulia mapafu.

Nipashe MWANGA WA JAMII
The Guardian www.ippmedia.com

## Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia wikiendi ijayo ya tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya Nipashe na The Guardian yatakuwa yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

# Karume hayupo lakini bado anaishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

## •Ni kutokana na fikra, falsafa na matendo mema kwa wananchi

LEO ni kumbukumbu ya miaka 52 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Zanzibar, mwanamapinduzi na Mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania. Huyu si mwingine bali ni ABEID AMANI KARUMEaliyeuawa Aprili 7, 1972.

Kiongozi na mwanamapinduzi huyo hayuko duniani zaidi ya nusu karne sasa lakini matendo yake na mema aliyoyafanya kwa ajili ya taifa yanamfanya aendelee kukumbukwa. Hiyo ni kutokana na alivyojitoa muhanga kwa ajili ya taifa lake la Zanzibar (lilivyokuwa wakati huo) kabla ya kujiunga na Tanganyika takribani miaka 60 iliyopita.



Abeid Amani Karume

Wakati wa uongozi wake, Karume alijenga upendo na umoja wa kitaifa, misingi bora ya kiuchumi, kuleta haki na kupambana na dhuluma dhidi ya wanyonge, hivyo kumuenzi kwa vitendo kama wanavyothamini Mapinduzi ya Zanzibar.

Pia ni jambo la kujivunia kwamba wakati Sheikh Karume akitimiza miaka 52 ya kifo chake, mambo mengi kati ya aliyokuwa akiyatamani kuyashuhudia yamefanyika au yanaendelea kufanyika.

Licha ya misukosuko ya hapa na pale iliyolikumba taifa ndani ya miaka 52 iliyopita, Zanzibar imebaki kuwa ya amani ya utulivu pia kukiwa na viashiria vyenye mwanga mwema katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kidemokrasia.

Wakati taifa likifanya kumbukizi ya miaka 52 ya kifo cha Sheikh Karume, wananchi wa Tanzania - Bara na Visiwani, hawana budi kuyaenzi mazuri aliyoyafanya na kujitafakari, hasa viongozi katika nafasi zao, ni alama gani watakazoziachia baada ya kumaliza mwendo kama Mzee karume.

**UCHUMI WA BULUU**

Moja ya falsafa ya Mzee Karume ambayo inaendelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya nane, chini ya Rais Dk. Hussein Mwinyi, ni sera ya uchumi wa buluu. Sera hiyo inaakisi ndoto za waasisi wote wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa manufaa ya Wazanzibari na watu wote duniani.

Kupitia Uchumi wa Buluu unaoangazia maendeleo ya utalii na rasilimali za bahari kama vile mafuta, uvuvi, kilimo cha mwani na majongoo bahari, wananchi wa Zanzibar wameanza kuona nuru na njozi za Mzee Karume zikitimia licha ya kwamba hayupo.

Kumekuwa na mageuzi makubwa kwa wananchi kupitia miradi hiyo ambayo inabadilisha kwa kasi Maisha ya wananchi kutoka katika umaskini Kwenda kwenye manufaa makubwa kiuchumi na kijamii.

**ARDHI NA MAKAZI**

Alama nyingine ambayo haiwezi kusahaulika Zanzibar iliyofanywa na Mzee Karume ni suala la ardhi kuwa mali ya serikali na kuondoa umiliki kutoka kwa wakoloni waliokuwa wakiishikilia na kuwafanya wananchi kuwa watumwa.

Karume alitamka wazi kuwa ardhi itakuwa chini ya serikali na itatolewa kwa wananchi kwa haki na usawa. Kutokana na jitihada hizo, wananchi walipewa ardhi kwa ajili ya matumzii ya kilimo na shughuli zingine za kiuchumi kwa manufaa yao. Kabla ya Mapinduzi, ardhi ilikuwa ikiwanufaisha watawala pekee.

Ujenzi wa nyumba za makazi kwa wananchi zikiwamo nyumba za maendeleo zilizojengwa eneo la Michenzani, Unguja

INAENDELEA UK. 8

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

KUMBUKUMBU

Bodi Ya Wakurugenzi, Uongozi Pamoja Na Wafanyakazi Wote Wa **Mamlaka Ya Mapato Zanzibar (ZRA)** Wanaungana Na Wananchi Wote Wa Zanzibar Katika Kumbukumbu Ya Kumuenzi Muasisi Wa Zanzibar Marehemu **Mzee Abeid Amani Karume.** Tukiwa Tunaadhimisha Miaka 52Tangu Kutokea Kifo Cha Jemedari Wetu, ZRA Inaungana Na Wazanzibari Wote Kwa Ujumla Kumkumbuka Kwa Uongozi Wake Wa Kishujaa, Busara Na Hekima Zake Katika Kuiongoza Zanzibar, Tunaendelea Kumuombea Dua Alale Mahala Pema. Mamlaka Ya Mapato Zanzibar Inaendelea Kuwasisitiza Wafanyabiashara Kuendelea Kuutumia Mfumo Wa Kutolea Risiti Za Kielektroniki Kila Wanapofanya Mauzo Kama Inavyoelekezwa Na Sheria. Aidha Mamlaka Ya Mapato Zanzibar Inawakumbusha Wananchi Wote Kwa Kukataa Kuuziwa Bidhaa Au Huduma Bila Ya Kupatiwa Risiti Za Kielektroniki Ili Serikali Iweze Kudhibiti Mianya Ya Upotevu Wa Mapato, Kodi Iweze Kusanywa Kwa Ufanisi Na Zanzibar Iweze Kufikia Tunu Na Shauku Ya Uchumi Wa Buluu.

"MUNGU AILAZE ROHO YA MAREHEMU KARUME MAHALI PEMA PEPONI.

1972 - 2024

"TULIPE KODI KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR"



Sheikh Abeid Amani Karume

Zanzibar Revenue Authority (ZRA),
P. O, BOX 2072, Mazizini- Zanzibar,Tel: 255-24-2230639/2233041,
Fax: 255-24-2233904, Email: zrb@zanrevenue.org

ZRA Pemba Office
S.L.P 163, Pemba, Zanzibar.
Tel: +255 24 2452553, Fax: +255 24 2452945

**HABARI KITAIFA**

# Mvua yasababisha maafa Kibiti kaya 3,000 zazingirwa na maji

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

KATA tano katika wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, zenye kaya 3,290 nyumba zao zimezingirwa na maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo, akizungumza kwa njia ya simu na mwandishi wa habari hii jana, alisema kata hizo ni zile zilizo karibu na Bonde la Mto Rufiji.

Alisema waathirika wa mafuriko hayo ni wakazi 19,740 ambao baadhi yao waliwahi kuondoka kabla ya mafuriko na wengine bado wanaendelea kuhamishwa na boti za maliasili.

Kanali Kolombo alisema kabla ya mafuriko hayo, Machi 3, mwaka huu, walipewa tahadhari kutoka uongozi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere wakitakiwa kuhama maeneo ya bondeni.

Hata hivyo, alisema wananchi wachache walifanikiwa kutoka katika eneo hilo baada ya taarifa, huku wengine wakiendelea na taratibu za kuhama hadi pale mafuriko yalipotokea.

Kanali Kolombo alisema kwa sasa msaada mkubwa unaohitajika ni wa mablaketi, dawa na vyakula, kwani mazao ya wananchi wengi yameathriwa na maji.

"Huo ndio msaada mkubwa kwa sasa ambao unahitajika ingawa muda mfupi uliopita nimepokea simu kutoka mkoani kwetu, wakisema wanaleta misaada kama hiyo kwa wahanga,"alisema.

Alifafanua kwamba wananchi wengi waliokumbwa na adha hiyo wote ni wakulima na wameenda katika maeneo hayo kwa shughuli za kilimo na kwamba, vijiji vinane na vitongoji 19 ndivyo viko katika bonde hilo.

Mbali ya makazi na mazao kuathiriwa na mafuriko pia, alisema huduma za kijamii zikiwamo shule tatu za msingi katika kata hizo zimezingirwa na maji na hivyo kukwamisha wanafunzi kuendelea na masomo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, alisema maeneo yaliyoathirika zaidi ni katika kata za Muhoro na Chumbi na hadi sasa kata 12 za makazi ya wananchi yamezingirwa na maji.

Meja Gowele alisema wanaendelea na tathmnini kwa kata zilizoathirika na mafuriko na kwa sasa, wamemaliza kata sita, watakapokamilisha zote watatoa taarifa kamili kwa kuwa, bado maji yanaongezeka na kupungua.

"Maji ni yale yanayotoka katika Bwawa la Mwalimu Nyerere baada ya kufunguliwa, lakini kwa mvua za mwaka huu, ilitakiwa kuwa na mafuriko makubwa sana kuanzia mwezi wa kwanza kwa hiyo, bwawa limetusaidia.

"Na kabla ya kufungua maji tulitoa taarifa kwa wananchi tukasimamia na ndiyo maana hujasikia vifo vilivyosababishwa na maji, bila kufanya hivyo, tungekuwa na maji mengi sana.

"Kwa kuwa, maji yanayotoka kwenye mito mingine kuingia Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mita 8,000 kwa sekunde na yanayoachiwa ni mita 3,000 mpaka 6,000. Kuwapo kwa bwawa ni nafuu," alisema.

# Waziri Mkenda aonya wanaorudisha wanafunzi kwa sababu ya michango

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekemea tabia ya baadhi ya walimu wa shule za msingi kuwarudisha nyumbani wanafunzi kutokana na wazazi kushindwa kulipa michango waliyojiwekea ikiwamo ya chakula.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitoa onyo hilo jana jijini hapa alipokuwa akifunga mkutano wa mwaka wa pamoja wa tathmini ya sekta ya elimu kwa mwaka 2023/24.

Prof. Mkenda alisema hakuna utaratibu wa kiserikali wa kumrudisha mwanafunzi nyumbani kwa kukosa michango kwa kuwa, dhana ya elimu bila ada inaelekeza mtoto asinyimwe kwenda shule kwa kukosa michango na kuwa, hakuna adhabu yoyote itakayofanya mtoto akose masomo.

Alisema katika sheria ndogo walizojiwekea za michango ikiwamo ya chakula, ni vyema wakawabana wazazi kama walivyokubaliana na si kuwarudisha watoto shule.

Prof. Mkenda alihimiza jamii kushiriki kikamilifu katika kuchangia chakula shuleni ili kuendelea kuiunga mkono serikali katika dhana yake ya elimu bila malipo.

"Suala la elimu bila malipo haina maana kuwa ni elimu bure kwa kuwa, wazazi mnanunua madaftari na vitu vingine vya kumwezesha mtoto kusoma kwa sababu serikali ilishafanyakazi kubwa ya kutoa elimu bila malipo.

"Jamii nayo ihamasike kuchangia baadhi ya michango ikiwamo chakula na isitokee mtoto akarudishwa nyumbani kisa hajalipa michango," alisema.

Awali, akisoma maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo, Kamishina wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema wajumbe mkutano huo wametoa maazimio 10 ikiwamo kuishauri serikali kuona umuhimu wa kutunga sheria itakayowalazimisha wazazi na walezi kuchangia chakula shuleni.

Alisema suala la huduma za chakula na lishe katika shule ni muhimu kwa wanafunzi ili kujenga afya ya akili.

Dk. Mtahabwa alisema wameshauri kuimarisha vikao vya tathmini ya utendaji katika sekta ya elimu ili viwe na matokeo chanya zaidi na kuitaka wizara kupeleka nyaraka zote muhimu kuhusu sera, mikataba ya utekelezaji, mitaala kwa watekelezaji wote, ili kuweza kurahisisha wadau wote kutekeleza kwa ufanisi.

Pia alisema wadau wameazimia kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na wadau wanaotoa elimu ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu, huku wakishauri kuongeza nguvu za kuwekeza katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

"Azimio jingine ni itafutwe mbinu na mikakati ya upatikanaje wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mbalimbali ya elimu na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya uwezeshaji na utekelezaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi," alisema.

Dk. Mtahabwa alisema wameazimia kuwapo na ushirikishwaji madhubuti jamii katika utoaji wa elimu na ushirikishwaji wa wadau kutoka mafunzo ya amali.


**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

**TANGAZO KONGAMANO LA KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS K. NYERERE LITAKALOFANYIKA TAREHE 8 APRILI 2024 KATIKA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere anapenda kuwaalika Viongozi na Wananchi mbalimbali kushiriki katika Kongamano Maalumu la kumkumbuka Muasisi wa Chuo hiki na Baba wa Taifa Mwalimu Julius. Kambarage Nyerere. Kongamano litakalofanyika siku ya Jumatatu Tarehe 8, Mwezi wa Nne mwaka wa 2024 katika Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Kivukoni Dar es Salaam- lenye mada kuu isemayo: "MCHANGO WA MWALIMU NYERERE KATIKA UONGOZI, AMANI, UMOJA NA UWAJIBIKAJI KWENYE UJENZI WA TAIFA".

Lengo la Kongamano hilo ni kumuenzi Baba wa Taifa katika mambo aliyopigania na kuyasimamia.

Mada mbili zitawasilishwa na watoa mada kama ifuatavyo:

Mada ya kwanza ni SIASA SAFI NA UONGOZI BORA KATIKA UJENZI WA TAIFA – hii itawasilishwa na Dkt.Ayoub Rioba Chacha ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na mada ya pili inayohusu AMANI, UMOJA NA UWAJIBIKAJI KATIKA UJENZI WA UTAIFA itawasilishwa na Kanali Mstaafu Joseph Leon Simbakalia ambaye amewahi pia kushika nafasi mbalimbali za Uongozi Serikalini.

Mwenyekiti wa mjadala wa Kongamano hili atakuwa: MH. PROF. PALAMAGAMBA KABUDI ambapo Mgeni Rasmi wa Kongamano hilo ni: MH. DKT. EMANUEL JOHN NCHIMBI- KATIBU MKUU WA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM)



*NYOTE MNAKARIBISHWA KATIKA KONGAMANO HILI IMETOLEWA NA: KITENGO CHA MAWASILIANO NA MASOKO-MNMA*

(022) 2820041/2820047 I 0736659965 (KIVUKONI CAMPUS)
(024)250315 I 07676846663 (KARUME CAMPUS)
(024)2452200 I 0777654770 (PEMBA CAMPUS)

rector@mnma.ac.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa mambo haya aliyoyafanya Karume ataendelea kuenziwa

**LEO** ni kumbukumbu ya miaka 52 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, aliyeuawa Aprili 7, 1972. Watanzania wanamkumbuka kiongozi huyo kwa mambo mengi aliyoyafanya kwa ajili ya Wazanzibari kwa kujitoa kwake kwa ajili ya ustawi wao.

Karume kwa kushirikiana na Wazanzibari wenzake, akiwamo Tito Okello, Ramadhani Haji Faki na Abdallah Said Natepe, walijitoa muhanga kuikomboa Zanzibar kwa kuongoza Mapinduzi Matukufu ya Januari 12, 1964 yaliyomng'oa Sultani visiwani humo.

Baada ya Mapinduzi hayo, Karume alitangaza kuwa Wazanzibari wote ni sawa bila kujali imani, rangi wala asili zao. Kutokana na hilo, alisema Mwafrika anaweza kumwoa Mwarabu na mhindi akamwoa Mwafrika au vinginevyo. Yote hiyo ni kuonyesha kuwa hakuna ubaguzi wa rangi miongoni mwa watu wa Zanzibar.

Jambo kubwa lingine aliloliweka hadharani ni usawa katika umiliki wa ardhi na maisha bora kwa wananchi wote. Alitangaza ardhi kuwa chini ya serikali na wananchi wote watapewa sehemu ili waitumie kwa ajili ya uzalishaji mali.

Sambamba na ardhi, alifanya kwa vitendo kuhakikisha wananchi wanakuwa na makazi bora kwa kujenga maghorofa, maarufu kama nyumba za maendeleo Michenzani, Unguja na kisiwani Pemba. Majengo hayo yaliwanufaisha wengi na hiyo ilionyesha kuwa kiongozi huyo alikuwa na dhamira ya dhati katika kuleta ustawi wa watu wa visiwa hivyo.

Karume pia hakupenda makuu wala madaraka makubwa na hiyo ilijidhihirisha mwaka 1964 alipokutana na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere na kukubaliana kuziunganisha nchi zao na kuwa na taifa moja. Karume alikubali na kujishusha kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania huku akimwachia Nyerere kuwa Rais.

Kiongozi na mwanamapinduzi huyo hayuko duniani zaidi ya nusu karne sasa lakini matendo yake na mema aliyoyafanya kwa ajili ya taifa yanamfanya aendelee kukumbukwa. Kwa matendo yake, Karume alijenga upendo na umoja wa kitaifa, misingi bora ya kiuchumi, kuleta haki na kupambana na dhuluma dhidi ya wanyonge.

Baada ya kufariki dunia, mambo mengi aliyokuwa akiyahimiza, ambayo yalikuwa njozi zake za juu ya Zanzibar anayoitaka kwa ustawi wa wananchi, yako mambo mengi yametekelezwa na yanaendelea kufanywa viongozi waliofuata baada yake. Mambo hayo yote yanaonekana katika sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, ardhi na makazi bora, kubwa zaidi, ni maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Moja ya falsafa ya Mzee Karume ambayo inaendelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya sasa, chini ya Rais Dk. Hussein Mwinyi, ni sera ya uchumi wa buluu ambayo inaakisi ndoto za Karume na waasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa manufaa ya Wazanzibari na watu wote duniani.


Kutokana na mazuri aliyoyafanya, kila inapokaribia kumbukizi yake, makongamano mbalimbali yamekuwa yakiandaliwa ikiwa ni sehemu ya kuenzi mchango wake huku mambo mbalimbali yakisisitizwa ikiwamo kujenga tabia ya uzalendo wa kuipenda nchi na maendeleo ambayo ni falsafa ya kiongozi huyo.

Wakati wa kongamano la mwaka huu lililoandaliwa na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere katika Kampasi ya Karume, Zanzibar, Rais Dk. Mwinyi, alisema fikra na falsafa za kimaendeleo na kizalendo za Mzee Karume hazina budi kuendelea kuenziwa kwa maslahi ya taifa.

Dk. Mwinyi aliweka bayana kuwa Mzee Karume alijenga upendo na umoja wa kitaifa, misingi bora ya kiuchumi, kuleta haki na kupambana na dhuluma dhidi ya wanyonge, hivyo Watanzania hawana budi kumuenzi kwa vitendo. Pia aliwasisitiza Watanzania kujikumbusha misingi ya utendaji wenye kuacha alama katika maisha kwa kuendeleza na kukuza uzalendo.

Kwa mambo aliyoyafanya ikiwamo kujitoa muhanga kwa ajili ya taifa bila kujali maslahi binafsi, Watanzania wanapaswa kumuenzi Mzee Karume. Viongozi kwa upande wao, wanapaswa kuiga nyayo zake kwa kujali maslahi ya wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mwenge wa Uhuru, wadau wawe uchaguzi wa serikali za mitaa

**MBIO** za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024, zilizinduliwa mkoani Kilimanjaro hivi karibuni na unatarajiwa kukimbizwa katika halmashauri 195 ndani ya mikoa 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kama ambavyo huwa inafanyika kila mwaka, mbizo hizo kwa mwaka huu zina kaulimbiu isemayo: "Tunza mazingira na shiriki uchaguzi wa serkali za mitaa kwa ujenzi wa taifa endelevu".

Uamuzi wa kuja na kaulimbiu hiyo, hasa ya kuhimiza wananchi kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, ninaweza kusema kuwa imekuja wakati sahihi, kutokana na kwamba mwaka huu ni wa uchaguzi huo.

Ninaamini, hatua ya serikali kuja na kaulimbiu hiyo ni baada ya kubaini uwapo wa baadhi ya wananchi, ambao huwa hawajishughulishi na masuala ya uchaguzi ingawa ni haki yao kuchagua au kuchaguliwa.

Kimsingi, katika uongozi wa kidemokrasia, ushiriki wa wananchi katika uchaguzi ni wa muhimu, kwa ajili ya kupata viongozi wanaotokana na ridhaa yao kuanzia ngazi ya msingi ya vitongoji, vijiji na mitaa.

Kwa hiyo kaulimbiu katika mbio za mwenge huo, inaweza kusaidia wananchi kujua nafasi yao katika jamii na kutambua ushiriki na ushirikishwaji kama njia ya kusaidia kupata viongozi kidemokrasia.

Lakini pamoja na hayo, ninadhani inahitajika kuongeza nguvu zaidi katika utoaji elimu ya mpiga kura na uraia inahitajika kwa kushirikisha wadau wengine ili elimu hiyo ienee kote.

Ninaeleza hivyo kwa sababu sidhani kama kupitia kaulimbiu hiyo tu, wananchi wote wanaweza kufikiwa na kupata elimu ya kutosha, hasa kutokana na kwamba si rahisi Mwenge huo kufika kila kijiji.

Mwenge utapita katika halmashauri 195, na sio kila kijiji, hivyo wakiwapo wadau wengine wa kusaidiana na serikali katika utoaji wa elimu, ninadhani elimu inaweza kusambaa kila kitongoji.

Kwa njia hiyo, watu wanaweza kuachana na kawaida yao kujiweka pembeni wakati wa uchaguzi na kuachana na kauli kwamba hawataki siasa, huku wakiwa wanaongozwa na viongozi wanaotokana na siasa.

Ziko sababu nyingi ambazo baadhi ya watu wamekuwa wakizitaja za kutoshiriki katika uchaguzi, lakini ni vyema kutambua kuwa ushiriki wa kila Mtanzania kwenye uchaguzi ni jambo la muhimu.

Lakini ninadhani yote hayo yanasababishwa na ukosefu wa elimu ya mpiga kura ambayo inatakiwa kutolewa kupitia vyombo vya habari vya taifa, binafsi na pia mashirika yasiyo ya kiserikali.

Ndiyo maana nikaeleza kuwa kuna haja kuruhusiwa kwa wadau wengi zaidi wa kutoa elimu badala ya kazi hiyo kufanywa na Mbio za Mwenge wa Uhuru ambazo haziwezi kufika kila kijiji.

Yako mashirika ya kiraia ambayo hujishughulisha na utoaji wa elimu ya mpiga kura, elimu ya uraia ili kuwajengea wananchi uelewa kuhusu umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Ninaamini kwamba kupitia kaulimbiu hiyo, huku wadau wengine wakishiriki kutoa elimu, wananchi wataelimishwa vya kutosha na kuona umuhimu wao kushiriki katika uchaguzi huo.

Kwa njia hiyo itakuwa ni rahisi wananchi kupata viongozi ambao wametokana na ridhaa yao, watakao waongoza kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwishoni mwa mwaka huu. Kutoshiriki katika uchaguzi, ni sawa na kutoa nafasi kwa wagombea wasiofaa kuchaguliwa na kusababisha malalamiko yakiwamo ya kutofanya kazi ipasavyo.

Ninaamini kwamba wananchi wakishiriki kikamilifu kuweka viongozi wanaowataka, itakuwa ni rahisi kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma katika vitongoji, vijiji na mitaa.

Vilevile, wataweza kufanya uamuzi katika vikao mbalimbali, kuhoji utendaji wa viongozi wao kupitia vikao mbalimbali, kuhamasisha uwazi katika mapato na matumizi ya rasilimali zilizoko katika maeneo yao.

Wananchi pia wanaweza kuwasimamia viongozi wao kupitia njia ya sanduku la kura, kwa kuchagua viongozi waadilifu na hata kuwaondoa madarakani kwa njia ya vikao halali iwapo si waadilifu.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Uwazi katika utenguzi, utumbuzi uwe kama ilivyo hisani ya uteuzi



Pascal Mayalla

Kitu kizuri zaidi, si tu Rais Samia anakwambia kwa nini amekuteua, bali anaelekeza uende ukafanye nini! Mfano, Paul Makonda amepewa kazi maalumu Arusha, jiji la kitalii, hivyo anapaswa kujikita kwenye kukuza utalii lakini pia kuna maelekezo mengine ya kuyashughulikia na kuwashughulikia yakiwamo masuala ya wale vijana wa RChuga na 'cha Arusha".

WIKI hii niliangalia tukio la uapisho wa wateule wapya wa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dar es Salaam. Katika uapisho huo, nilifarijika sana kuona miongoni mwa waalikwa wa tukio lile ni Mzee wa Ngomeni, Richard Mwasha, kwa jina maarufu la Kuhani Musa.

Nimefarijika sana kumuona Rais Samia akitoa sababu za kumteua kila aliyemteua na kumpa majukumu kwa uwazi kabisa.

Enzi za Kikwete, Tanzania ilitia saini ule mkakati wa 'Open Government Initiative' uliokuwa unasisitiza ukweli na uwazi (truth and transparency). Dk. John Magufuli, maarufu kama JPM, alipoingia madarakani aliufuta mkakati huo. Hata 'Bunge Live' likafutwa, mikutano ya vyama vya siasa ikapigwa marufuku na hata mikutano ya ndani kuzuiwa.

Rais Samia alipoingia na falsafa yake ya 4R, akafanya mabadiliko mengi makubwa ikiwamo kufungulia mikutano ya siasa.

Kwa mujibu wa Katiba Jamhiri ya Muungano wa Tanzania ( JMT), Rais wa JMT anaweza kushauriwa na wasaidizi wake lakini kwenye kufikia uamuzi, anafikia hatua hiyo yeye kama yeye. Halazimiki kufuata ushauri wa mtu yeyote na hawajibiki kutoa sababu yoyote kutokana na uamuzi aliochukua.

Mamlaka na nguvu za Rais kuteua na kutengua zinaitwa 'discretionary powers' kwa kuteua, kutengua au kutumbua bila kutaa sababu yoyote kwa yeyote. Kwa hiyo kitendo cha Rais Samia kuwa muwazi na mkweli kwa kutoa sababu za kumtea fulani mahali fulani na kumpa majukumu kwa uwazi, ni hisani kubwa na nzuri kwa mustakabali mwema wa nchi yetu.

Anachokifanya Rais Samia kuwa muwazi, sababu za kuwateua wateule wake, ni hisani tu tena hata uapisho mubashara kisha kutolewa hotuba, kulianza na JPM. Zamani hatukuwahi kuwa na hotuba kwenye uapisho. Ni kuapa tu ndivyo iliyokuwa.

Kitu kizuri zaidi, si tu Rais Samia anakwambia kwa nini amekuteua, bali anaelekeza uende ukafanye nini! Mfano, Paul Makonda amepewa kazi maalumu Arusha, jiji la kitalii, hivyo anapaswa kujikita kwenye kukuza utalii lakini pia kuna maelekezo mengine ya kuyashughulikia na kuwashughulikia yakiwamo masuala ya wale vijana wa RChuga na 'cha Arusha".

Yule wa Mara ambaye ni mjeshi, kaelekezwa kwenda kushughulikia kijeshi jeshi kile kilimo cha lile zao (hakulitaja) ambalo Mara ni maarufu na kulivusha mpakani na nchi jirani.

Hiki anachofanya Ras Samia ni sawa na ile 'Open Government Initiative' kwa mteuliwa kupewa changamoto waziwazi na kwa ukweli, akishindwa kutekeleza hayo, jamii nzima itajua hivyo, Hiki ni kitu kizuri kwa uwajibikaji.

Tanzania tuna sheria ya haki ya kupata habari au kupata taarifa, hivyo wananchi kuelezwa kila kinachowahusu ni haki yao na sio hisani.

Kwa vile Rais Samia ameshaonyesha njia kwa kutuhisania, tuwe watu wa shukrani. Kwanza, kwa kumshukuru kwa hiyo hisani, kisha tumwombe atupe na haki ya kupata taarifa. Asiishie kwenye kutupatia taarifa za uteuzi tu bali pia tupatiwe na taarifa za sababu za utenguzi kwa sababu maofisa hao ni watumishi wa umma, wanaolipwa kwa fedha za umma, hivyo umma una haki zote za kujua kuhusu utendaji wa wateule hao na sababu za kutenguliwa kwao na kutumbuliwa.

Mfano Makonda, baada ya kuteuliwa Mwenezi wa CCM, amefanya maajabu katika kipindi kifupi na kurejesha imani ya wananchi kwa CCM kwa kuwakimbiza viongozi mchakamchaka, wengi wakitaraji mchakamchaka huo ungeendelea hadi mwaka 2025 katika uchaguzi mkuu, aingie bungeni na kupewa wizara nyeti, lakini ghafla akatumbuliwa na kupewa nafasi ya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Mtu yeyote mwenye cheo kikubwa, akaondolewa na kuteuliwa cheo kidogo ni kutumbuliwa tu, hivyo Makonda ametumbuliwa uenezi na kupoozwa na ukuu wa mkoa. Dk. Bashiru Ally Kakurwa, alitumbuliwa ukatibu mkuu kiongozi na kupewa ubunge na kilemba cha ubalozi. Kwa hiyo, kama ilivyo sifa njema kuteuliwa, mtumishi wa umma akiborongа kisha kutumbuliwa , umma uelezwe sababu za kufikiwa kwa hatua hiyo.

Kwa maoni yangu, nafasi za juu zote wakiwamo wakuu wa mihimili- Jaji Mkuu, Spika wa Bunge na wakuu wa taasisi za serikali zinazojitegemea, nafasi zinapokuwa wazi, Watanzania wenye sifa waombe, washindanishwe tupate mwenye sifa na uwezo kuliko wengine ndipo Rais apelekewe na kuteua badala ya utaratibu wa sasa wa watu kuteuliwa na baada ya siku mbili kutenguliwa. Haileti picha nzuri sana kwa awamu hii ya Rais Samia.

Nchi nyingi wakiwamo jirani zetu Kenya, Jaji Mkuu anaomba kazi, anasailiwa kisha kupatikana aliye bora na ndiye anayeteuliwa. Nimalizie kwa kumpongeza tena Rais Samia kwa kutuhisania uwazi na ukweli kwenye uteuzi anaoufanya na hii tuifanye kuwa haki na si hisani.

**Wasalaam**
**Paskali**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ligi Kuu ya Siasa na mambo ndani ya Sisiemu FC



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HII Ligi Kuu ya Siasa inayoendelea nchini kwa miaka kadhaa sasa, hakika inapamba moto hata kufanya klabu bingwa ya mara zote nchini, Sisiemu FC kuonyesha ikifanya kila juhudi katika kufukuzia kutwaa kwa mara nyingine Kombe la Ubingwa mwakani.

Hivi sasa, Ligi inaelekeaelekea ukingoni, huku Klabu bingwa hiyo ikionekana kubadilisha wachezaji wengi katika kila mechi, huku timu shindani zikiendelea kubaki na wachezaji wale wale kwa mechi zote, lakini pengine ni kwa nia nzuri ya kutwaa ubingwa tena.

Kila Sisiemu FC inapopambana na mshindi ambaye pia ni wa mara zote Chadema FC, imekuwa ikitolewa jasho kutokana na mshindani wake huyo kudumu na wachezaji wake kwa muda mrefu, tofauti na Wazalendo FC ambayo hivi karibuni iliachana na nahodha wake na kupata mpya.

Ziko timu zingine kama Kafu FC na Mageuzi FC ambazo zimekuwa zikionekana kama washiriki tu ambao hakuna hata mwaka zimekuwa tishio kwa Sisiemu FC ambayo inaonekana kuwatia jambajamba washiriki wengine wa ligi.

Klabu zingine kama Yuemudii FC, Tadea FC, Chauma FC na kadhalika, zimekuwa zikisubiri Sisiemu FC atwae ubingwa ili nazo zijisogeze karibu kushangilia na kushiriki karamu zinazoandaliwa na mabingwa hao.

Kwa miaka mitatu iliyopita, Sisiemu FC imefanya mabadiliko katika safu yake hususan ya ushambuliaji kwa kuwabadilishabadilisha huyu na yule lakini ikishindwa kujiamini na kufanya isikae muda mrefu ikihofia kukabiliana na mavetereani Chadema FC wakiongozwa na nahodha wake mkongwe, Freeman Mbowe.

Sisiemu FC baada ya kumbadilisha nafasi mshambuliaji wake kiongozi, Abdulrahman Kinana, na kuwa kocha msaidizi, ilimteua Daniel Chongolo ambaye kutokana na uchezaji wake, akishambulia kwa kasi kutoka kushoto na kujizolea sifa, wenzake walimfitini na yeye kuamua kubwaga manyanga na akimpisha kiungo hatari, Emmanuel Nchimbi aliyekuwa kwa muda mrefu akicheza soka la kulipwa nje.

Lakini wakati akijiandaa kuiunganisha timu, kocha mkuu akamwibua mchezaji mwingine, kiungo wa kati, Paul Makonda, aliyekuja kwa kasi kubwa akitokea mchangani na kuanza kushambulia hata goli la timu yake badala ya kupeleka mpira mbele.

Mabao ya kujifunga katika timu yakazidi, hivyo kocha kuona ampumzishe na kumpeleka kikosi cha pili, huku akimpandisha Amos Makalla kutoka kikosi cha pili kushika nafasi hiyo. Kwa wanaomfahamu wanasema atazиba pengo barabara.

Ili kujipanga barabara, kocha mkuu akaona bora pia ampandishe kijana mwingine, Ally Hapi, kutoka timu za mikoani ambaye anakumbukwa wakati fulani mazoezini alipata kushambulia makocha wastaafu wa timu waliotaka kushauri jambo la ushindi, akiwataka waache kuweweseka.

Baadhi ya wapenzi na wanachama wa klabu ya Sisiemu FC, hata hivyo, wanaonekana kuridhishwa sana na muunganiko wa Makalla na Nchimbi kuwa unaweza kuivusha timu ikaendelea kutwaa Kombe la Ubingwa mwakani, lakini wakisema watapata kipimo halisi katika nusu fainali inayotarajiwa kuchezwa baadaye mwaka huu.

Hata hivyo, kuhusu mchezaji mwingine, John Mongela, wanasema ni mpole kiasi cha kuingiwa hofu kama ataweza kumkaba beki matata wa Chadema FC, Benson Kigaila au beki wa kati, John Heche, ambaye ameichezea timu hiyo kwa takriban miaka yote ya uhai wake.

Ukweli ni kwamba Klabu ya Sisiemu FC imekuwa haitulii katika kujipanga na kubaki na kikosi kile kile kitakachoimarika na kuzoeana na kumpunguzia kazi kocha mkuu kwani ni kama kila baada ya mechi hutafutwa wachezaji wengine na kubadilishana na waliopo.

Mwaka huu na mwaka ujao ni wa uchaguzi, nchi ikianza na uchaguzi wa serikali za mitaa mwishoni mwa mwaka huu,na hatimaye uchaguzi mkuu mwakani ambao ndio hasa utakaoamua ni nani atapata nini katika mbio za kusaka mlango wa Ikulu, bungeni na kwenye mabaraza ya madiwani.

Sisiemu FC imekuwa ikihaha kutokana na kupoteza utaratibu wake wa zamani wa kuwa na kambi nzuri za mafunzo na mazoezi kwa timu yake ya wakubwa lakini pia kukosa vituo vya vijana na kusababisha kuokoteza wachezaji.

Ikumbukwe, enzi za Mwalimu Nyerere, kulikuwa na vyuo vya mafunzo ya itikadi kwa vijana ambao ndio walikuja kuwa viongozi wa baadaye; kina Jakaya Kikwete, Edward Lowassa, William Lukuvi, Dk Nchimbi, John Guninita, Sukwa Saidi Sukwa na wengineo wengi.

Leo kama hakuna anayepelekwa katika vyuo hivyo kwa maandalizi ya uongozi wa baadaye, Sisiemu FC itaishia kufanya majaribio ya wachezaji na hatimaye Chadema FC ambayo imekaa na wachezaji wake kwa siku nyingi itatwaa Kombe la Ligi Kuu ya Siasa. Uchaguzi Oyeee!

# TANAPA yaibuka na ushindi tuzo za umahiri

**Na Halfani Chusi**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kupitia Idara ya Mawasiliano limeibuka mshindi katika tuzo za Umahiri katika Mawasiliano ya Umma zilizotolewa juzi mkoani Dar es Salaam.

Tuzo hizo zilizobeba dhima ya "The Best Use of Influencers Category for the Year 2023", zilitolewa na Chama cha Maofisa Uhusiano na Mawasiliano Tanzania (PRST).

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Mkuu wa Mawasiliano wa TANAPA, Catherine Mbena, alisema ushindi huo umetokana na mchango mkubwa unaotolewa na idara yake katika kuhabarisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya uhifadhi na utalii.

Alisema idara hiyo imekuwa daraja la kuiunganisha taasisi hiyo na umma, na kwamba tuzo hiyo itakuwa chachu ya kuimarisha uhusiano kati ya TANAPA, serikali, vyombo vya habari na wadau mbalimbali.

"TANAPA sasa ni jicho la nchi kwa kuwa, taasisi inatoa mchango mkubwa wa kuingiza fedha za kigeni na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kasi kupitia sekta ya utalii. "Tunatoa shukrani za dhati kwa serikali kwa kuongeza hamasa katika sekta ya utalii na kutangaza kimataifa kupitia Filamu ya The Royal Tour," alisema.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliipongeza (PRST) kwa kuandaa tuzo hizo ambazo zinachochea uwajibikaji. Alisema ni muhimu kwa waandishi wa habari na maofisa uhusiano kwa umma kuongeza ubunifu, weledi na uwajibikaji ili jamiii inufaike kwa kupata taarifa sahihi zinazohusu maendeleo ya taifa.

Alisema tuzo hizo zitasaidia kkuza vipaji na kuongeza chachu kwa wanataaluma akiwataka waandaji wake kutenda haki na kwa kufuata misingi na taratibu zilizowekwa.

# Othman alia watumishi kukosa uadilifu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema pamoja na Zanzibar kuendelea kuhitaji wataalamu zaidi katika fani mbalimbali, bado kuna tatizo kwa baadhi ya wataalamu na wasomi kukosa uadilifu katika utumishi.

Othman aliyasema hayo juzi baada ya futari ya pamoja na viongozi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Lumumba walioko kambini kujitayarisha na mitihani ya kidato cha sita inayotarajiwa kufanyika mapema mwezi ujao.

Alisema baadhi ya wasomi walioko katika utumishi, wamekuwa wakikosa uadilifu na uzalendo kwa kufanya ubadhirifu wa mali za umma pamoja na kuendekeza rushwa jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya nchi

Makamu wa kwanza wa Rais aliwataka wanafunzi hao kujiandaa katika kutenda uandilifu na kuwa wazalendo wa kweli kwenye dhamana mbalimbali watakazokabidiwa na kuendelea kuitumikia vyema nchi yao.

Kwa mujibu wa Othman, kwa kufanya hivyo, watakuwa mfano mwema katika juhudi za pamoja za kuijenga Zanzibar na kuleta maendeleo kwa manufaa ya wananchi wote.

Alisema shule ya Lumumba ndicho kitovu cha elimu Zanzibar chenye historia kubwa katika kutoa wataalamu na wasomi wengi wa sekta mbalimbali nchini, hivyo ni alama kubwa ya elimu kwa Zanzibar na inahitaji kutunzwa.

Othman aliwataka walimu na viongozi wizara kwa ujumla, kuendelea kuitendea haki alama hiyo ya elimu kwa Zanzibar kwa kuonyesha kuwapo wataalamu bora wenye madili mema kwak uwa Lumumba ndio mtambo na kiwanda muhimu cha kuzalisha wataalaamu hao.Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Said, akitoa salamu baada ya futari hiyo, alisema serikali imekuwa ikichukua juudi kubwa katika kutoa kipaumbele kwenye uwekezaji wa sekta ya elimu hasa ujenzi wa madarasa na vifaa vya kufundisia pamoja na ajira kwa walini.

Alisema hatua hiyo imeonyesha kuwapo dalili kubwa za kupatikana mabadiliko ya kimaendeleo katika sekta ya elimu Zanzibar.

Pia alisema ufaulu wa wanafunzi wa michepuo na vipawa umeonezeka kuanzia mwaka 2021 kutoka wanafunzi 2,200 hadi wanafunzi 6,600 kiasi ambacho ni onezeko la mara tatu la zaidi ya mafanikio jambo ambalo limechangiwa kwa kuwapo juudi kubwa za walimu katika kuwafundisha wanafunzi wao.

Mkuu wa Shule hiyo, Mussa Hassan, alisema ujio wa wa viongozi wakuu katika shule hiyo ni motisha kwa walimu kuendelea kuhamasika kufanya kazi kwa bidii na pia ni deni kwa wanafunzi kujitaidi katika masomo yao ili kuendelea kufanya vyema na kupata matokeo mazuri.

Alisema viongozi wanafahamu kwamba Lumumba ni shule iliyowekezwa sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi kielimu Zanzibar.

Naye Mwanaarabu Said Mbwana, kwa niaba ya wanafunzi wenzake, alimshukuru Othman kwa uamuazi huo wa kufutari nao pamoja na kuahidi kwamba watafanya kila juhudi katika masomo ili malengo yao ya kufaulu katika kiwango cha daraja la juu yafanikiwe.

# Karume hayupo lakini bado anaishi

**INATOKA UK, 4**

utamfanya Karume akumbukwe kwa azma ya kuwafanya wananchi kukaa katika nyumba bora. Nyumba kama hizo ziko pia kisiwani Pemba.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Rahma Kassim Ali, anasema serikali itaendelea kumuenzi Sheikh Karume kwa kujenga na kuzikarabati nyumba za maendeleo ambazo zimejengwa katika kipindi cha uongozi wake mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 1964.

Anasema Hayati Sheikh Karume baada ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 alianza kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za maendeleo kwa ajili ya wananchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama cha Afro Shiraz (ASP) kuwapatia wananchi wake makazi bora.

Ujenzi wa nyumba za maendeleo, anasema ulifanyika pia katika eneo la Kikwajuni chini ya msaada wa wataalamu kutoka katika nchi iliyokuwa ikifahamika Ujarumani Mashariki.

"Wizara tutaendelea kuunga mkono juhudi kubwa zilizochukuliwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, za kuzifanyia ukarabati nyumba za maendeleo ambazo zimejengwa katika kipindi chake kwa lengo la kuwapatia wananchi makazi bora yenye stara," anasema.

Aidha, anasema majengo mengi yapo katika hali ya uchakavu mkubwa kiasi cha kupotezа haiba yake kwa sababu hayajafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Aadhi ya majengo hayo nio nyumba za Vitongoji, Pemba tayari wakazi wake wamelazimika kuhamishwa baada ya kuharibika vibaya na kusababisha kuta zake kufanya nyufa kubwa hali ambayo ni hatari kwa usalama wa wananchi.



Abeid Amani Karume

mambo mengine ambayo yaliasisiwa na Hayati Karume na yanaendelezwa na serikali iliyoko madarakani ni pamoja na kuwaenzi wazee kwa kuwapatia makazi bora na kuwalipa pensheni jamii. Hayati Karume alijenga nyumba kwa ajili ya makazi bora ya wazee mwaka 1969 eneo la Sebleni, Unguja pamoja na kuwapatia pensheni ya kujikimu ikiwa sehemu ya kutambua mchango wao mkubwa kwa ukombozi wa Zanzibar.

Kwa sasa Serikali ya Zanzibar imeongeza malipo ya pensheni jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 kwa kulipwa Sh. 50,000 kila mwezi.

**VIJANA WAMUENZI**

Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi Mstaafu, katika kumuenzi Mzee Karume, anawasihi vijana kujenga tabia ya uzalendo wa kuipenda nchi na maendeleo ambayo ilikuwa miongoni mwa mambo yaliyomo katika falsafa ya kiongozi huyo mwasisi wa Zanzibar na Muungano.

Anasema wakati Zanzibar ikifikisha miaka 52 bila ya Mzee Karume, yako mambo mengi ya kujifunza ikiwamo uzalendo wa kupenda nchi pamoja na utekelezaji wa ahadi za wananchi ambazo ndizo zilizochochea hamasa ya kumwondowa mkoloni.

"Baada ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964, Hayati Karume pamoja na viongozi wenzake, walianza kutekeleza ilani ya uchaguzi ya ASP ambayo azma kubwa ilikuwa kuharakisha maendeleo na kustawisha hali za wananchi kuwa sawa," anasema Nahodha.

Pia anasema katika kipindi kifupi cha uongozi wake, ujenzi wa nyumba bora za kisasa za kuishi wananchi ulifanyika kuanzia mjini hadi vijijini huku wananchi wakipewa nyumba hizo na kuishi bure.

"Viongozi wa sasa waliokabidhiwa madaraka na tuliong'atuka, tunatakiwa kuishi kwa kufuata mambo mazuri yenye maslahi kwa wananchi ambayo yalitekelezwa na kusimamiwa kikamilifu na Hayati Karume ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa manifesto (ilani) ya chama kilichokuwa kikitafuta uhuru cha ASP ambacho ni ahadi ya wananchi na chama," anasema.

**MJANE WA KARUME**

Mama Fatma Karume, mjane wa mwasisi huyo wa Zanzibar na Muungano, anazitaja sifa kubwa za Hayati Karume katika kipindi alichoishi naye kuwa ni kuwapenda watu na kujali utu na mapenzi makubwa yenye bashasha. Anasema baada ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 Mzee Karume alitangaza kugawa eka tatu tatu za ardhi kwa wananchi wote kwa ajili ya kutoa nafasi ya shughuli za kilimo na makazi.

"Hadi Karume anafariki dunia mwaka 1972, alifanikiwa kugawa zaidi ya ekari 97,000 za ardhi kwa ajili ya kilimo. Yeye hakuchukua hata nusu ekari. Karume hakuwa na ubinafsi wa kupenda kujimilikisha mali au ardhi," anasema.

Alisema mashamba hayo ya ardhi waliyopatiwa wananchi bado baadhi wanayaendeleza kwa shughuli za kilimo.

**AHADI YA DK. MWINYI**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza hivi karibuni katika Kongamano la Sita la Kumbukumbu ya Karume lililofanyika katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Karume, Zanzibar, alisema wananchi wanapaswa kuzienzi na kuziendeleza fikra na falsafa za kimaendeleo na kizalendo za Hayati Sheikh Karume kwa maslahi ya taifa.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, Dk. Mwinyi alisema Mzee Karume alijenga upendo na umoja wa kitaifa, misingi bora ya kiuchumi, kuleta haki na kupambana na dhuluma dhidi ya wanyonge, hivyo kumuenzi kwa vitendo kama wanavyothamini Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kutimia kwa miaka 52 ya kumbukizi ya Mzee Karume ni vyema Watanzania kujikumbusha misingi ya utendaji wenye kuacha alama katika maisha na mifumo katika serikali kwa kuendeleza na kukuza uzalendo miongoni mwao.

Alisisitiza kuwa ni vyema jamii ikakumbuka na kurejea katika misingi ya falsafa za uwazi, uadilifu, ushirikishwaji, amani, upendo na ubunifu na utendaji wenye kuboresha maisha ya wananchi.

# MAISHA

APRILI 7, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

## Juisi ya Pera



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Nyumba bora ni pamoja na hewa safi



Ukurasa 12

## HARUSI





# MAJANI YA MPERA Kiboko ya nywele

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | S | H | I | N | A |
| D | | | | M | | N |
| I | | D | U | A | | Z |
| W | A | O | | R | A | I |
| A | | N | I | A | | S |
| N | | D | | | | H |
| I | B | A | R | A | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ZAA, MIA, TII, NAE, MBATA, MEZWA, SIMBA, AMANI, ASHINDE, UBINGWA


## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

TAFUTA MAUMBO HAYA KATIKA MCHORO ULIOPO HAPO CHINI.






## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ushuhuda wa kutisha mchawi akimwaga siri

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kupata mauzauza ya dunia yetu hii. Wachawi waanza kutoa siri zao hadharani baada ya mambo kuwawia magumu. Sikiliza ushuhuda huu ufungue macho yako ya kimwili na kiroho.

Watu wengi wamekuwa wakipuuzia kuhusu habari za uchawi eti kwamba haupo. Wanaugua, wanaachishwa kazi, wanakosa kazi, wanafilisika japo walikuwa matajiri wakubwa. Mbaya zaidi, wanakufa vifo vya ghafla. Lakini bado wanaona ni matukio ya kawaida kumbe chanzo ni maadui waliojificha.

Adui aliyejificha ni hatari kuliko mtu anavyofikiri. Yule adui unayemjua na kumwona ni rahisi kumshughulikia, hata kumkwepa kwa tahadhari. Mara nyingi nimeeleza hapa kwamba kuna ulimwengu wa aina mbili, huu unaoonekana kwa macho ya mwili na ule wa roho usioonekana.

Ulimwengu usioonekana ndio hatari zaidi na ndiko chimbuko la matatizo yote. Huanzia huko ndiko matatizo yakajidhihirisha kwa kuyaona kwa macho ya mwili.

Leo tuweke suala la ndoa kando tukisubiri maoni kwa tuliyojadili wiki zilizopita. Tuangaze sarakasi za wachawi katika ulimwengu wa roho (ule uliojificha), hauonekani lakini yanayofanyika huko ni makubwa na ya kutisha.

> **Simba alikuwa anakula kwa mwaka na alikuwa anafanya mawindo kwani wakati nazaliwa chui, nyoka walikuwa silaha kwa ajili ya vita kwa sababu mimi nilizaliwa katika familia ya kitemi.**

Wiki moja iliyopita nilihudhuria kongamano la injili pale viwanja wa Biafra, Kinondoni mkoani Dar es Salaam. Kiongozi wake alikuwa Mchungaji Ezekiel kutoka Kenya. Ni kongamano la siku nne lililokuwa na miujiza na shuhuda mbalimbali.

Ushuhuda ulionigusa sana ni baba mmoja wa hapa Tanzania aliyejisalimisha Machi 22, mwaka huu, akaelezea mambo ya kichawi aliyofanya katika maisha yake hadi kusababisha kukatwa mguu baada ya kukiuka masharti kwa wakuu wake wa kichawi.

Hebu sikia sehemu ya maelezo yake niliyobahatika kuyanasa ili ujue wachawi wapo na wanafanya mambo makubwa ya kutisha. Bwana huyu anasema hivi;-

"Ndugu zangu waliniloga sana. Wakaniambia mtoe mtoto wako wa kwanza, ama mama yako au baba yako. Lakini mimi niliposhirikishwa jambo hilo nilikataa. Baada ya kukataa ndugu zangu waliniloga sana.

"Baada ya hapo walinishambulia sana wachawi, wakadai kwamba kila baada ya mwaka nitakuwa naletewa gunia 20 za mahindi, gunia tano za maharage na Sh. 500,000 kila mwaka. Lakini bado nilikataa kwa sababu walitaka niwe mwenyekiti ili niweze kutoa sadaka ya watoto. Lakini kwa bahati nzuri kwa sababu katika ukoo wetu tulikuwa wachawi wakubwa. Ndiyo maana wale walinitamani ili niwe mchawi katika kikundi chao.

"Na bahati nzuri katika kuishi, nilizaliwa nikakuta chui, simba, chatu, nyoka weusi, nyuki wa ndani. Nyuki nilikuwa nawafuga ndani, halafu na vyura waikubwa sana ambao wakilia tu najua kwamba kesho lazima mvua inyeshe. Wakilia tangu asubuhi hadi jioni, najua kesho itanyesha mvua ya mafuriko na wakilia mara moja, najua kwamba kesho kutakuwa na mvua za muda wa saa moja.

Alipoulizwa na Mchungaji Ezekiel kwamba wanyama hao walikuwa wanakula nini akasema; "Nyoka wanakula unga na mimi ndiye ninayewapa. Ezekiel: Ulikuwa na nyoka wangapi? Akajibu alikuwa na nyoka wengi sana.

Akasema vyura walikuwa wanakula wadudu na walikuwa wanaishi chini ya kitanda na chini ya mtungi wa maji. Nyoka niliwajengea nyumba ya milango minne. Simba na chui tulikuwa tunamchinjia kondoo, mbuzi mweupe na kuku mweupe kila baada ya mwaka.

Simba alikuwa anakula kwa mwaka na alikuwa anafanya mawindo kwani wakati nazaliwa chui, nyoka walikuwa silaha kwa ajili ya vita kwa sababu mimi nilizaliwa katika familia ya kitemi.

Kukiwa na vita anaenda simba, chui au nyuki. Hivyo ni vita vya kiuchawi pale ufalme na ufalme ukitaka kugombana ulimwengu wa giza. Tunatuma simba au nyoka au nyuki. Lakini kwa bahati nzuri mimi nilianza kuwatumia kwa kwa kulipiza kisasi.

Mtu akija kunipa Sh. milioni mbili au tatu basi natumia nyuki au fisi. Lakini kwa bahati mbaya mwaka 2018 mwezi wa 11 nikawa nimeugua kiuno, nikachomwa sindano. Baada ya muda tatizo likatokea, damu ikavimba kuanzia kiunoni upande wa mguu ule uliochomwa sindano. Nikapata kitu walichoita ni 'gangri', nikakatwa mguu.

Msomaji wangu, fuatilia wiki ijayo mambo mazito mbele. Baada ya kukatwa mguu, nini kiliendelea? Tafuta nguvu ya Mungu mpendwa kudhibiti wachawi. ***Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581. Namba ipo pia WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Wanavuja machozi kisa vijana hawaoi, hakuna watoto wanaozaliwa

IKO kasumba ya vijana hivi sasa kutotaka kuoa na wengine kuolewa, wakiishia kuamini kuwa 'single mother' ni bora zaidi ya kuishi na mume.

Kauli zao siku zote ni kwamba "siwezi kuoa kama sina vitu vya thamani ndani. Hata wanawake wa sasa, ni ngumu kukubali kuolewa na mwanamume asiye na kitu.

"Kwa umri wangu, si kama sitaki kuoa, lakini siwezi kuingia kwenye ndoa kama sina gari, nyumba, biashara, kitanda, jokofu, kabati na vitu vingine vya thamani."

Basi katika kutafuta mali pamoja na mwanamke atakayemuoa, vijana walio wengi wanaeleza bila kumung'unya maneno kwamba hakuna mwanamke anayeweza kumvumilia mwanamume asiye na kitu ndiyo maana nao hawataki kuoa.

Wanaoijua Biblia, kupitia kitabu cha Ayubu 15:20 imeandika: "Mtu mwovu huwa na uchungu siku zake zote, hata hesabu ya miaka aliyowekewa mwenye kuonea." Kwa maana hiyo, uchungu husababisha mambo ya mtu kuwa magumu na uchungu husababisha kufikiri machungu zaidi kuliko mema.

Jambo lingine ni ulevi uliopindukia. Watu wanasahau kwamba uamuzi wao wa kutotaka kufanya kazi za uzalishaji mali na kujikita katika ulevi kucha kutwa, nalo ni kiini cha kupoteza nguvu na uwezo wa kuwa na mwanamke.

Nimeanza kuleza hayo kwa sababu ya jambo linaloumiza kichwa. Huko Mwika Kaskazini, Jimbo la Vunjo, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, inadaiwa ndoa ni hadithi nyingine.

Serikali ya eneo hilo imekiri hadharani kwamba hakuna vijana wanaooa, wala watoto wanaozaliwa Mwika Kaskazini kwa sasa kutokana na mambo mbalimbali yanayochangia tatizo hilo. Ni hali ya kustaajabisha inayoelezwa na Ofisa Mtendaji Kijiji (VEO) cha Msae-Kinyamvuo katika Kata ya Mwika Kaskazini, Elizabeth Mkony.

Kutokana na tishio hilo, Halmashauri ya Kijiji kwa kushirikiana na viongozi wa dini, wamekubaliana kuja na mpango kabambe wa kupambana na changamoto ya kuporomoka kwa maadili, kunakosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya na pombe kupita kiasi.

"Sasa hivi, Mwika Kaskazini hakuna vijana wanaooa wala watoto wanaozaliwa. Kanisani nako kwa mwaka mzima unakuta si zaidi ya watoto watatu wanatangazwa kuzaliwa na kubatizwa.

"Tumefikia hatua ambayo jamii inaumia, wengine wana kufa vifo vya ajabu kwa sababu ya ulevi. Vijana wanashindwa kufanya kazi za kujitolea kwa sababu ya kukosa nguvu.

"Kutokana na hali hii kushamiri, kama uongozi wa kijiji pamoja na viongozi wa dini kufanya jambo, ili kuwanusuru vijana wetu na kuongeza uzazi. Kwa vile tunaona kwa miaka miwili ijayo, kuna uwezako wa kukosa vijana."

Badhi ya mambo yanayowekewa mkazo na timu hiyo ya pamoja, ni kutoa elimu na kukemea ulevi kupindukia, ubakaji, ulawiti, unyanyasaji wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya na wanafunzi kukatisha masomo.

Kabla ya kutangazwa kwa azimio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Wilbad Mariki, anasema: "Hakuna namna, imebidi tukae na viongozi wa dini na kuweka mikakati ya jinsi ya kupambana na hali mbaya iliyopo.

"Kata nzima ina watu 19,000 hata 30,000 hatujaikaribia. Tunazidi kuporomoka, tunaona tusipopambana wote kwa pamoja kuona mambo yanaenda vizuri, hatutakuwa na kizazi kinachofanya kazi," anasema.

Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Mwongai wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Neema Malisa, anasema wakiwa viongozi wa dini wameanza kuchukua hatua kwa nafasi yao.

"Tunawafundisha watu wetu faida za kumpenda Mungu, na hasara za kujiingiza katika matendo maovu kama ushoga, ulawiti, ulevi, ubakaji na matumizi ya dawa za kulevya.

"Ni vile tu mtu hawezi kuona, lakini tunaumizwa sana na mambo mabaya yanayotendeka katika jamii. Tuko tayari kuungana na serikali kuhakikisha mambo maovu na haramu hayaingii kwenye kijiji chetu.

"Mnafurahi watoto wetu wanapokufa, mnafurahi watoto wetu wanapoacha kuoa na kujikuta wanaingia kwenye ushoga na ulawiti? mimi naona tuiunge mkono serikali. Sisi viongozi wa dini tuko tayari," anasema Mchungaji Malisa.

Kwa kweli hali hii nim baya na iwapo itaachwa jinsi ilivyo, kuna hatari ya jamii kukosa kizazi. Si kizazi tu bali kizazi madhubuti ambacho kitaendeleza kupeleka mbele gurudumu la maendeeo. Mungu atusaidie.

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI





Kumbukumbu isiyofutika kwa Msonge Msilanga wakati akifurahia siku yake ya kuagwa na familia yake Julai 27, mwaka 2022 katika Ukumbi wa Prime Rose, Mbezi mkoani Dar es Salaam. Msonge alifunga ndoa na Yusuf Kaoneka Julai 29,2022





# MITINDO

## FURAHIA EIDD

# Tupia abaya

WAKATI zimebaki siku chache kabla ya watu kufurahia sikukuu ya Idd El Fitr kwa kula vyakula vitamu na kuvaa nguo za kupendeza.

Hata hivyo, wakati huu wengi wanaumiza vichwa vyao kujua aina gani ya nguo wanaweza kuvaa ili watoke tofauti zaidi.

Kulingana na mazingira halisi vazi la abaya ni chaguo zuri kutokana na kuwa na mwonekano mzuri na wenye stara.

Vazi hili la abaya ambalo ni baibui la kisasa zaidi, lina heshima yake na huvalika kila mahali pasi kujali ni aina eneo unalotaka kwenda.

Mitindo ya vazi hili linaongeza vionjo katika mwonekano wake, kwani kuna abaya mviringo, kipepeo na hata mchanganyiko wa mitindo.

Katika sikuu ya Eidd, wanawake wengi wanaopenda mavazi ya stara wanavaa vazi hilo.

Faida ya vazi la abaya linamfanya mtu kupemndeza zaidi hasa ikiwa na rangi nyeusi au yoyote ya kung'aa.

Asili ya vazi hili ni nchi za uarabuni, Uturuki na hapa Tanzania lilianza kuhsmiri sehemu za pwani, lakini sasa kila mahali linapendwa kuvaliwa.






## UREMBO

Na Mary Geofrey









MAJANI YA MPERA

# Kiboko ya nywele

MAJANI ya mpera yana vitamin B ambayo ni kirutubisho kizuri cha nywele.

Bidhaa nyingi za nywele zinayatumia kutokana na faida zake na pia wengine wanameza vidonge vyenye kirutubisho cha biotini..

Majani ya mpera ambayo yana vitamin B na C, katika nywele yanatumika kwa njia ya aina mbili, ambazo ni kupulizia chai ya mpera na kuvukiza.

HAIR TEA

Maana yake huoshi ukishapulizia kwenye nywele yako kwenye ngozi na juu

Kwakuwa lengo letu ni kuipa nywele unyevu na chai au maji ya mpera ni mazuri kwa njia hii kwa sababu yanasaidia kuilinda ngozi isipate maradhi kama mba na fangasi.

Pia yanarudisha rangi ya nywele ambayo imepotea na wenye mvi pia inakusaidia, nywele kukua vizuri na inaipa afya.

Ni kilainishi kizuri unakupopuliza ma kisha kupaka mafuta juu hata kama umesuka.

**JINSI YA KUFUKIZA**

Chemsha majani ya mpera kama unachemsha chai ya rangi, ikichemka iache ipoe kisha weka kwenye chupa ya kupulizia.

Ukishapulizia maji yako paka mafuta kwenye nywele na hii ni kama chai inakaa salama siku moja au siku mbili bila kuharibika. Iwapo utahifadhi kwenye friji unaweza kutumia wiki nzima.

Tumia kwa muda mrefu zaidi angalau hata miezi mitatu na utashuhudia mabadiliko mazuri ya nywele zako.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya Pera

MAPERA ni matunda yanayopatikana kwa wingi lakini mara nyingi huwa hayapendwi kuliwa kutokana na ugumu wake wakati wa kuyatafuna.

Mapera pia yanafaa kutengeneza juisi kwa ajili ya kunywa ikiwa imechanganywa na pasheni.

**Mahitaji**

Kwanza kabisa andaa mapera matano makubwa yaliyoiva vizuri, pasheni tisa zilizoiva, sukari kiasi na maji kiasi kwa ajili ya kuandaa juisi yako.

**Namna ya kutayarisha**

Anza kwa kuosha osha na katakata mapera kisha tia katika mashine ya kusagia na usage ukiweka maji kiasi, kabla ya kuichuja vizuri.

Katakata pasheni toa nyama yake, halafu saga katika mashine na changanya na juisi ya mapera.

Weka sukari kiasi kadiri upendavyo ikiwa tayari itakuwa juisi imekamilika, hapo unaweza kunywa na kitafunwa chochote kile.





MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Nyumba bora ni pamoja na hewa safi









KUNA misemo mbalimbali katika Maisha ya kika siku kuhusu nyumba. Mara utasikia nyumba choo bwana! Mara nyumba mapambo na mengine mengi. Yote hayo ni kuonyesha umuhimu wa nyumba bora kwa maisha bora na afya pia.

Katika safu hii ninakuletea msemo mwingine kwamba nyumba bora ni ile iliyotengenezewa mifumo mizuri ya uingizaji wa hewa ndani. Nyumba inapokosa mifumo mizuri ya kuingiza hewa, hapo ndipo na vichafua hewa ndani huanza kujijenga.

Changamoto kubwa iko zaidi kwenye nyumba za kisasa kutokana na nyingi kuzibwa kila mahali jambo ambalo limeonekana kuwa la kawaida hasa milango na madirisha vinapokuwa vimefungwa kwa muda mrefu kuliko vinavyofunguliwa.

Njia rahisi ya kuondoa tatizo hili ni kufungua madirisha kila siku pamoja na kuhakikisha nyumba inafanyiwa usafi katika kila njia ya nyumba ambayo ni chanzo cha kuingiza hewa.

Jambo lingine ni kuzingatia usafi wa jumla wa nyumba nzima kwamba sakafu ziwe safi na zisafishwe kila inapobidi.

Kutokuruhusu taka, nguo chafu, vumbi na uchafu mwingine kujijenga kwa sababu unakaribisha uwezekano wa kuharibu hali ya hewa ndani ya nyumba. Hata katika chunmba cha kulala, m5tu anatakiwa kuhakikisha kuna vitu vichache kama vile nguo ili kuruhusu nafasi na hewa safi.

Kutoruhusu vyombo vichafu vijazane kwa muda mrefu bila kusafishwa pia kuepuka kuhifadhi nguo chafu kwa muda mrefu bila kufuliwa na kufuta fumbi kila wakati ni jambo la muhimu.

Pia kama unavyo vifaa vya kisasa vihusianavyo na maboresho ya hewa ya ndani kama vile viyoyozi na feni, hakikisha vinafanyiwa usafi wa mara kwa mara ili machujio yake yasibebe vumbi na kushiriki kulisambaza.

Sababu nyingine inayochangia uwapo wa hewa nzito na chafu ndani ya nyumba ni uvutaji wa sigara ndani. Hili ni jambo baya ambalo linapaswa kupigwa marufuku kwa kuwa husababisha athari kubwa kiafya.

Hewa hiyo binadamu anahitaji aipate katika kila mahali anapokuwapo iwe ni sehamu pa kazi, nyumbani na kwingineko.

Kutokana na umuhimu huo wa hewa kwa binadamu, nyumbani napo ambapo ni mahali muhimu anapotumia muda wake mwingi, panahitajika pawe na hewa ya kutosha, si tu hewa lakini pia iwe safi.

Wakati mwingine unaweza ukaingia ndani ya nyumba ukakutana na hewa nzito ambayo ukikaa muda mfupi, unahisi maumivu ya kichwa kwa mbali.

Binadamu tunatofautiana. Wako ambao wana uwezo mkubwa wa kuhisi kitu chochote ambacho hakiko sawa kwa haraka ndani ya nyumba hasa upande wa harufu au kunapokosekana hewa nzuri na safi.

Matatizo hayo ya uwapo wa hewa mbaya ndani ya nyumba, yanaweza kusababishia wanafamilia matatizo ya kiafya endapo hakutakuwa na ufumbuzi wake au jitihada za kuweka mazingira ya nyumba kuingiza hewa safi.

Inawezekana mwanzoni likaonekana ni jambo gumu la kufanya lakini ukweli ni kwamba kuboresha hali ya hewa ya ndani ni rahisi sana. Unachotakiwa ni kuzingatia tu mambo machache na unaweza kuwa na nyumba huru isiyo na harufu na isiyokuwa na vichafua hewa.

DONDOO

Na Restuta James

# Ipambe sehemu ya kulia chakula kwa sinki zuri

NIPASHE ambayo imetembelea maduka tofauti jijini Dar es Salaama, imebaini kuwa 'mchawi' wa aina hiyo mpya ya sinki ni bei kwani ni kubwa ikilinganishwa na ya udongo yaliyozoeleka.



SINKI la kunawia mikono linatajwa kuwa sehemu ya pambo katika eneo la kulia chakula. Hii ni kutokana na mwonekano na muundo wake.

Mtaalamu wa mapambo ndani, Winnie Joseph, ameiambia NIPASHE katika mahojiano maalumu kwamba kumekuwa na miundo mipya ya kuvutia inayoendelea kuvumbuliwa na wana teknolojia.

Anasema katika sehemu ya chakula, imekuja miundo mipya kuanzia kwenye ramani ya ujenzi wa nyumba hadi nakshi zinazokamilisha eneo hilo.

Anasema moja ya pambo linaloongeza thamani na mwonekano wa eneo hilo ni sinki la kunawia mikono.


"Wavumbuzi wamekuja na design (muundo), mpya wa kisasa ambao unaleta uhalisia (natural), ndani ya nyumba. Sinki la kunawia la jiwe lililopolishiwa vizuri kama unavyoona," anasema Winnie akionesha baadhi ya masinki hayo.

Anasema kitu pekee kinachovutia kwenye muundo huo ni utulivu (calmness), unaoletwa na sinki hilo.

Winnie anasema masinki hayo yanapatikana kwa rangi tofauti tofauti ikiwamo nyeusi, kahawia na kijivu.

Hata hivyo, anasema muundo huo haujafuta yale ya udongo ambayo yanatumika hivi sasa kwani bado kuna watu wanaopendelea aina hiyo.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...SHIBE NI FARAJA YA MUDA...

## HABARI KIMATAIFA

# Guterres aonya Israel kutumia akili bandia

**NEWYORK,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, amesema ana wasiwasi kuhusu taarifa ya uchunguzi inayoonyesha jeshi la Israel, linatumia akili bandia kutekeleza mashambulizi yake katika Ukanda wa Gaza.

Kauli ya Guterres inakuja siku chache baada ya nchi ya Marekani kusema inafuatilia kwa umakini madai ya ripoti za vyombo vya habari kwamba Israel imekuwa ikitumia akili ya kubuni kuisaidia kuchagua maeneo ya kushambulia.

Hata hivyo, msemaji wa Ikulu ya White House, John Kirby, alisema nchi yake bado haina uthibitisho wa undani kuhusu ripoti hiyo ambayo inataja kwamba Israel inatumia mfumo wa akili ya kubuni yenye uangalizi mdogo wa kibinadamu.

Hata hivyo, jeshi la Ulinzi la Israel limekanusha madai hayo.

Wakati huo huo, jeshi hilo lilisema limepata mwili wa mwanamume mmoja ambaye alitekwa nyara na kuzuiliwa eneo la Gaza.

Taarifa hiyo ilisema kuwa mwili huo ulipatikana jana wakati wa uvamizi wa kijeshi katika mji wa Khan Younis.

Mtu huyo aliyetambulika kwa jina la Elad Katzir alitekwa kutoka mji wa Kibbutz Nir Oz, wakati wa shambulizi la kushtukiza lililofanywa na kundi la Hamas kwenye eneo la kusini mwa Israel Oktoba 7, mwaka juzi.

Kulingana na Mamlaka ya usalama nchini humo(ISA), mwili huo ulipatikana ndani ya Gaza katika opereshi iliyofanyika usiku kucha na kurejeshwa nchini Israel.

Baada ya kufanyiwa uchunguzi ulitambuliwa na wahudumu wa matibabu na familia yake.

Jeshi hilo na ISA lilisema katika taarifa ya pamoja, kwamba Elad Katzir ambaye kulingana na taarifa za kijasusi, aliuawa akiwa amezuiliwa na kundi la kigaidi la Islamic Jihad.

Walisema kwamba mwili huo ulitambuliwa kwa kutumia taarifa za kina za kijasusi.

Katzir (47), alitekwa kutoka Niir Oz kwa pamoja na mama yake, Hanna, mwenye umri wa miaka 77.

Taarifa kutoka katika vyombo hivyo ilisema mama yake aliachiliwa huru Novemba mwaka jana, huku baba yake Avraham aliuawa katika eneo la Kibbutz.

Aidha, Kundi la Hamas lilisema jana kwamba ujumbe wake utatua leo nchini Misri kwa ajili ya vikao vya kujadili kusitishwa kwa mapigano Ukanda wa Gaza.

Ujumbe huo unaoongozwa na Naibu Mkuu wa kundi hilo, Khalil Al-Hayya, utahudhuria kikao hicho katika hatua ya kuitikia mwaliko kutoka kwa wapatanishi.

Hata hivyo, Hamas iliwasilisha masharti yake ambayo yalitolewa mwezi uliopita yenye mapendekezo 14 yaliyoandaliwa kabla ya maafikiano ya baraza la usalama wa umoja wa mataifa kupitishwa Machi 25.

**DW/BBC**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres. **PICHA: MTANDAO**

## Watu sita wauawa Kharkiv

**KYIV,** UKRAINE

WATU sita wameuawa katika mji wa Kharkiv nchini Ukraine baada ya kutokea shambulizi la ndege zisizo na rubani kutoka jeshi la Russia.

Meya wa mji huo, Ihor Terekhov alisema ndege hizo aina ya Shahed zilizotengenezwa na Iran zilishambulia majengo kadhaa, ikiwa ni pamoja na majengo ya ghorofa la makazi.

Mashambulizi dhidi ya mji wa Kharkiv, ulioko karibu zaidi na mpaka wa Russia, yameongezeka katika wiki za hivi karibuni.

Maofisa wa Ukraine walisema mji huo unaweza kuwa shabaha ya mashambulizi yanayofuata kutoka Russia.

"Shambulio hili dhidi ya wakazi wenye amani wa Kharkiv kwa mara nyingine tena linathibitisha kwamba Russia ni taifa la kigaidi," alisema Terekhov kupitia mtandao wa Telegram.

Katika tukio hilo, watu 10 walijeruhiwa na kufikishwa hospitali.

Picha ambazo hazijathibitishwa zilizochapishwa na polisi wa Ukraine, zilionyesha waokoaji wakiwa kwenye eneo la tukio, huku majengo yakiwaka moto baada ya shambulio hilo.

**BBC**

## Majimbo Somalia yakataa kufunga balozi za Ethiopia

**MOGADISHU,** SOMALIA

MAJIMBO mawili ya Puntland na Somaliland yamekataa kuzifunga balozi ndogo za nchi ya Ethiopia katika ardhi zao, kama ilivyotakiwa na serikali ya shirikisho la Somalia.

Somalia iliagiza balozi wa Ethiopia kuondoka ndani ya saa 72 kwenye ardhi yake kuanzia Alhamis na kumrejesha nyumbani balozi wake anayefanya kazi mjini Addis Ababa kwa mashauriano.

Hata hivyo, serikali ya Somalia ilitangaza kufungwa ndani ya wiki moja kwa balozi ndogo za Ethiopia katika mikoa ya kaskazini ya Puntland na Somaliland. Serikali ya Puntland, ambayo ilijitangazia uhuru wake mwaka 1998, na ipo katikati ya mgogoro huo ilisema haitaridhia uamuzi wa kufunga ubalozi mdogo katika mji wa Garowe.

Ilielezea uamuzi huu hautatekelezeka kutokana na serikali ya shirikisho ya Somalia kufuta katiba ambayo ilizingatia umoja wa kitaifa siku chache baada ya jimbo hilo kutangaza kwamba haitambui tena taasisi za serikali ya shirikisho ya Somalia. Jimbo lililojitenga la Somaliland, lilijitangazia uhuru wake kutoka kwa Somalia mwaka 1991 lakini halitambuliki na jumuiya ya kimataifa,. "Ubalozi wa Ethiopia katika Jamhuri ya Somaliland haukufungaliwa awali kwa idhini ya Somalia na kwa hivyo hautafungwa," Wizara ya Habari ya Somaliland ilisema katika taarifa yake.

Somaliland na Ethiopia wamejikuta katika mgogoro huo baada ya jimbo hilo kutangaza kutiwa saini itifaki ya mkataba unaotoa ruhusa ya ukodishaji wa kilomita 20 za ufuo wa Somaliland kwa Ethiopia kwa miaka 50. Mogadishu ilishutumu makubaliano hayo na kuyaita haramu na ukiukwaji wa uhuru wake. Serikali ya Ethiopia imesema kwamba itafanya tathmini ya kina kwa nia ya kuchukua msimamo kuhusu juhudi za Somaliland kutaka kutambuliwa.

Somalia imekataa juhudi zozote za upatanishi na Ethiopia hadi itakapojiondoa kwenye makubaliano na Somaliland.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ABERN ANDREW AKYOO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 509 APY,** CHASSIS NAMBA: **F300S003770** na ENGINE NAMBA: **HD0296208.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/9057/2024**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**ANDREW EDWARD TESHA**
Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0389_0037** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHAURITANGA SEKONDARI** mwaka 2006. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi **PHQ/MOR/ULA/7892/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**NDUGU FELIX AMSON MWAMBOGO** MKAZI WA JIJI LA MBEYA AMEPOTEZA KADI YA PIKIPIKI ILIYOSAJILIWA KWA NAMBA **T694 BKW.** AMERIPOTI KITUO CHA POLISI MBEYA NA KUPEWA HATI YA UTHIBITISHO **PHQ/MBE/7504/2024.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**SELELINA MAHENDEKA BUZUNE**
Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2365/0026** Kilichotolewa na **ANDREW FAZA MEMORIAL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MDL/K/B.1/1/VOL.1/107**

SAFU

MAKALA

# TUMIA MITANDAO YA KIJAMII HUKU UKIITAZAMA KESHO YAKO



Na Magabilo Masambu

**Mipango ya Mungu ni mikubwa huwa anamwinua yeyote. Unaweza kuwa mchekeshaji leo kama Steve Nyerere kesho ukawa Rais wa nchi kama alivyo Rais wa Ukraine, Volodyymyr Zelensky. Unawezab kuwa mchezaji mzuri wa mpira leo kama Mbwana Samatta, kesho ukawa Rais kama George Weah wa Liberia.**

NI kweli kwamba mitandao ya kijamii kama facebook, Twitter, Youtube, Whatsapp na Instagram, imerahisisha sana mawasiliano yetu. Leo kwa kutumia mitandao hiyo, tunaweza kuwasiliana na mtu yeyote duniani. Tunaweza kutuma ujumbe (sms), kutuma picha ama video au kupiga simu na kufanya mazungumzo.

Nje ya mawasiliano, wako wanaoitumia mitandao hiyo kibiashara ama kuuza bidhaa zao moja kwa moja, kutangaza au kufanya mawasiliano na wafanyabiashara wengine duniani. Lakini pia inatumika kuonyesha uwezo na vipawa vyetu. Mfano, kama una kipawa cha uimbaji, uigizaji, uandishi, siasa na kila aina ya sanaa, unaweza kuwaonyesha watu uwezo wako kirahisi.

Kinachosikitisha ni kwamba, pamoja na faida zote hizo, wako wanaoamua kwa hiari yao kutumia mitandao ya kijamii kinyume cha maadili yetu ya Watanzania ama kwa kujua au kwa kutojua madhara yake ya leo na kesho. Wanatuma picha au video za utupu mitandaoni bila kujali kwamba wana ndugu, jamaa na marafiki watakaozitazama.

Jambo ambalo hatulijui ni kwamba maisha ya mwanadamu ni fumbo kubwa kwa sababu tunajua tulikotoka lakini hakuna yeyote anayejua tunakokwenda. Kwa manenio mengine, hakuna anayeijua kesho yake. Tunaweza kudhani kwamba tulipo tumefika kumbe Mungu ana mipango mingine na sisi. Wako watu ambao wanajiona waimbaji, waigizaji, wachekeshaji, waandishi na kadhalika na wamejiridhisha kwamba maisha yao yatakuwa hayo.

Mipango ya Mungu ni mikubwa huwa anamwinua yeyote. Unaweza kuwa mchekeshaji leo kama Steve Nyerere kesho ukawa Rais wa nchi kama alivyo Rais wa Ukraine, Volodyymyr Zelensky. Unawezab kuwa mchezaji mzuri wa mpira leo kama Mbwana Samatta, kesho ukawa Rais kama George Weah wa Liberia.

Unaweza kuwa mwanamitindo leo kama Hamisa Mobeto kesho ukawa Jokate Mwegelo. Unaweza kuwa mwanamziki leo kama Giggy Money kesho ukawa mbunge kama Mwana FA. Wako wengi ambao walikuwa watu wa kawaida lakini wamekuwa maarufu na wameshika nafasi nyeti. Kwa mantiki hiyo, yeyote anaweza kuwa chochote.

Ninachotaka kusema ni kwamba nafasi tulizo nazo leo tusione hatuwezi kuwa wengine kesho. Kwa maana hiyo, matukio tunayoyafanya tukiwa na nafasi tulizo nazo leo, tuyafanye tukiwa waangalifu kwamba kesho na keshokutwa tukiwa watu mashuhuri kwenye jamii, mambo yetu ya leo yasitufanye tukahukumiwa kesho. Ni mjinga tu atakayehukumiwa kesho utetezi ukawa kwamba, nilifanya hayo kwa sababu nilikuwa msanii au ililinilazimu kufanya hayo kwa wakati huo. Lazima tutambue kwamba mitandao ya kijamii inahifadhi taarifa zetu milele.

Leo unapiga picha au video za utupu unazituma mtandaoni, kesho unakuwa Rais kama kijana wa Senegal au mtu mashuhuri. Waungwana wanakukumbusha kwamba kuna kapicha kako hapa unakakumbuka? Unaanza kutumia vyombo vya usalama kuwaumiza wanaokukumbusha kwa mambo ulioyafanya mwenyewe ukiwa na akili timamu. Nani atalaumiwa katika hilo kama si mwenyewe utajilaumu?

Nakubali kwamba kwa sababu ya ukuwaji wa teknolojia, inawezekana ukarekodiwa bila kuwa na taarifa lakini uzoefu unaonyesha wengi wamekuwa wakijirekodi na kupiga picha wenyewe au kuwaamini watu wao wa karibu na kwamba watazitunza. Lakini inapotokea kutokuelewana, wanaona silaha ya kukumaliza ni kuachia picha na video zako. Ni muhimu sana kujilinda kabla ya kulindwa na wengine. Linda utu wako lakini zaidi heshima yako ya leo na kesho.

Wako wanaotumia picha zao kuongeza watazamaniji (viewers) kwenye mitandao yao ya kijamii na inawezekana inawapatia fedha. Kwa maoni yangu, bado una uwezo wa kuongeza watazamaji kwa kulinda maadii, utamaduni na utu wako kwa sababu si watazamaji wote wanafurahia kuona picha za utupu. Fedha zinazopatikana kwa njia hiyo, hazitakuwa tofauti na za ukahaba au uuzaji wa bangi.

Jambo ambalo wengi pia hawajalifahamu ni kwamba le hii watu wengi wanakosa kazi duniani kwa sababu tu wamekuwa watumiaji wabaya wa mitandao ya kijamii. Unakwenda kuomba kazi kwenye kampuni fulani, una vigezo vyote vya kielimu lakini wanaotaka kukupatia kazi wanaona wajiridhishe kwa kulitafuta jina lako kwenye mitandao, wanakuta mambo ya ovyo! Maana yake wanaona wakikupatia kazi, unaweza kuharibu taswira ya kampuni yao. Wanaamua kutokuchukua pamoja na kwamba unazo sifa za msingi.

Ushauri wangu kwa watumiaji wenzangu wa mitandao ya kijamii, ni muhimu matumizi yetu ya leo yalinde heshima yetu ya kesho. Tunaweza kuwa na watoto wadogo leo kesho watakuwa watu wazima.

Tutawapa taabu sana watakapokuwa na wenzao au wenyewe kuzitazama picha na video zetu. Ishi leo kwa matarajio ya kuwapo kesho. Kazi yako leo isiuwe matumaini ya kuwa mtu mwingine kesho kwa kuwa lolote linawezekana bali ni jambo la muda tu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa cha jamaa aliyefumaniwa, akiruka ukuta na kutimua mbio*



Na Adam Fungamwango

**Matokeo yake, kumbe yuko mtu labda ni mume au mpenzi ambaye yeye ndiye anayelipa kodi, anagharimia na anayejulikana mitaa ile. Yeyote aliyekwenda hapo lazima atapata shida, kwa sababu kitu kinachoendelea hapo ni kufumaniwa na kuitiwa mwizi.**

KUNA baadhi ya wanaume wana akili za ajabu sana. Inakuwaje unaambiwa na mwanamke njoo nyumbani unakwenda kichwa kichwa? Hujawahi kufika hata siku moja nyumbani kwake. Hujui mazingira yake. Unaambiwa tu ni nyumbani kwangu, nyumba yangu au kodi analipa yeye, wewe unakwenda tu?

Baadhi ya wanaume wanashindwa kujiongeza kama nyuma ya pazia ya mwanamke huyo hakuna mfadhili ambaye anamlipia kodi. Au kuna mtu anayefika pale mara kwa mara na kuzoeleka.

Hivi kwa nini mwanamume unapokubaliana na mwanamke usitafute sehemu ambayo utakuwa uko huru kwenda naye? Sehemu ambayo hutakuwa na hofu ya kitu chochote, ikiwamo usalama wako?

Nasema hivi kwa sababu yameshawakuta wanaume wengi kupata matatizo makubwa pale walikubali kwenda nyumbani kwa wapenzi wao wa kike.

Kumbe baadhi wanakuwa si waaminifu, wameolewa na wengine wanaishi na wapenzi wao lakini ila kwa wakati huo, wanakuwa wamesafiri au wako mazingira ya nje na nyumbani.

Kwa bahati mbaya, baadhi wamefumaniwa, wamejeruhiwa kwa kupigwa baada ya kuitiwa wezi, na hata kuuawa. Kwa mwanamume, ni hatari sana unapokutana na mwanamke, akamwambia njoo nyumbani hakuna shida, akamwamini kwa asilimia 100.

Nadhani umeshawahi kuona au kusikia taarifa mbalimbali za wanaume wanaofumaniwa baada ya kwenda nyumbani wanakoishi wanawake, baada ya kuambiwa anaishi peke yake na hakuna shida.

Matokeo yake, kumbe yuko mtu labda ni mume au mpenzi ambaye yeye ndiye anayelipa kodi, anagharimia na anayejulikana mitaa ile. Yeyote aliyekwenda hapo lazima atapata shida, kwa sababu kitu kinachoendelea hapo ni kufumaniwa na kuitiwa mwizi.

Hii ya kuitiwa mwizi ndiyo mbaya sana kwa sababu raia wanapotoka huko huwa hawaulizi. Wanapiga tu, mwisho wake ni kujeruhi au kuua kabisa.

Mara nyingi wanaofumania wao kelele zao huwa ni za mwizi kwa sababu wanaamini mbaya wake atapata taabu na adhabu zaidi kuliko akisema amemfumania. Kwenye mambo ya kufumania, mara nyingi wao hawana mpango nayo sana lakini huku kwenye wizi ni balaa, hawana utani.

Mbali na kupigwa na raia, baadhi wa wanaofumania wamekuwa na hasira, wanaweza kufanya kitu chochote kile kibaya ikiwemo kukutia kilema cha maisha au kupoteza maisha yako kabisa. Wanaume wenye tabia hiyo, waache mara moja kabla hawajakutana na kitu kibaya.

Na hii haikuanza leo. Iko tangu miaka mingi iliyopita na kuna walioukutana na madhara, kama wanavyosimuliwa wanamuziki.

Hamed Maneti, akiwa na bendi ya Vijana Jazz, alitunga wimbo akauita 'Niliruka Ukuta' ambao unazungumzia kisa kilichomkumba alipokwenda kwa mwanamke aliyemdanganya hajaolewa. Wimbo huu unaimbwa hivi;-

"Nenda upesi, nenda ukamwambie, tokea leo asinifuate fuate, kitendo kile alichonitendea, kingenipo nza nipoteze maisha, kunidanganya kwamba hajaolewa na chumba kile amekipanga yeye, kumbe muongo, alinidanya, ilipofika saa nane ya usiku, nikasikia hido hodi fungua, bahati nzuri, nikaruka ukuta."

Huyu jamaa aliingizwa chaka na demu, akaenda kumbe mwanamke ana bwana! Saa nane tu jamaa akatinga.

"Kama ukifika mwambie ajurekebishe, mambo kama yale mabaya na yana hatari.

Kusema kweli si vibaya na wala si dhambi. Ya nini sasa kunificha na kunidanganga?

Nimeponea chupuchupu nashukuru Mungu. Kama si kuruka ukuta ingekuwa hatari.

Maisha yangu yangekwisha sababu ya yeye. Ya nini sasa kunificha na kunidanganya?"

Hapa inaonyesha jamaa amekutana na mtu anayemfahamu vyema mwanamke huyo. Sasa anampa salamu, akamwambia kitu alichokifanya ni cha hatari sana na asirudie tena.

Mwanamuziki Moreno Batamba, akiwa na bendi yake ya Orchestra Moja One ya nchini Kenya, naye alitunga kibao kinachofanana na hicho, akakiita 'Vituko Majengo.'

Unaimbwa hivi: "Nimekata shauri Majengo sitarudi, nilipata vituko kwa Fatuma Majengo. Nilitembea huko mgeni wa heshima, akanikaribisha chapati na mchuzi. Akanikaribisha karibu mgeni, nami nikaamini hakuna matata.

"Usiku wa manane nikasikia ngo ngo ngo, Fatuma kanifinya, kumbe ni sigino. Nikasita kidogo nikasikia ku ku, kumbe ni mwenye nyumba, nitajificha wapi? Mlango ukafunguka ukanikosea, nilitupiwa kiti nikasikia kuu, nikaumia sana nikatoka spidi, nikasahu shati, viatu na 'kabati.' Yeye hakutosheka akanifuata tu, nikaongeza spidi, kila kona ananifuata tu."

Nadhani hapa yoyote mwenye tabia hii ya kuwafuata wanawake nyumbani kwao atakuwa amejifunza kitu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba aliyomwelekeza aende kumuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, saa chache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-2

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

BAADA ya kupambana kwa muda mrefu, sasa anaendesha maisha yake kutokana na kuuza viatu vya mitumba pale kwenye kituo cha Chanika.

Hufanya kazi hiyo jioni na usiku, kwa kutandika turubai kando ya barabara na kuvimwaga, kabla ya kuitia wateja.

Kazi hii angalau ilimwingizia kipato cha kujikimu mwenyewe, ikiwa ni pamoja na kuweza kulipia kodi ya nyumba, kula na kuvaa kwa kiasi alichojaaliwa. Alipanga chumba kimoja.

Chumba chake kilikuwa cha uani, kikiwa moja kati vyumba vitatu vilivyokuwa uani, vilivyounganishwa kwenye safu moja, na mbele yake kubebwa na nyumba kubwa nyingine ya vyumba sita, maeneo ya Chanika.

Ilishatimu saa sita kamili mchana na katika kunusa aligundua kuwa harufu ile haikuwa ya kitu kingine zaidi ya panya aliyekufa.

Hapo aliona sasa kuna kazi kubwa ya kufanya. Nayo ni kumsaka panya huyo na kumtoa ili mpenzi wake akiwasili asikutane na harufu hiyo kwani ni aibu kubwa.

Hakukuwa na kingine chochote zaidi ya kupekua chumba chote ili kumsaka, ingawa kwa anavyojua haitokuwa kazi rahisi.

Akili yake ilimtuma kwanza aanze kwenye sanduku ambalo alikuwa ameweka nguo zake.

Akalifungua. Hakukuwa na harufu yoyote ambayo ilifanana na ile anayoisikia.

Akaliendea lile sanduku lake kuukuu ambalo anasubiri gari la taka ili alibebe awapelekee kwa kwenda kulitupa.

Kwa mara ya kwanza pesa yake ya takataka sasa itakuwa imekwenda kihalali, kwa sababu wanalazimishwa kulipa shilingi elfu tatu kwa watu wote waliopanga kwenye nyumba ile.

Pamoja na kulalamika yeye na mwenzake mmoja kuwa hawazalishi taka, kwani hawashindi nyumbani, hawapiki chakula, lakini si mwenye nyumba, mjumbe wala Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa aliyewasikiliza.

Pesa hiyo ililipwa kwa kila mmoja, aliye na watoto 10 hadi ambaye hana, aliyeoa hadi asiyeoa, anayepika nyumbani na hata asiyepika pia.

Ile kulifungua tu, akapiga chafya. Si kwa sababu ya ile harufu bali vumbi. Lilikuwa ni sanduku la zamani, ambalo aliweka nguo zake kuukuu ambazo kwa sasa hazitumii, lakini pia kulikuwa na viatu na ndala ambazo ameshaanza kuvitumia.

Akaanza kuchambua kitu kimoja baada ya kingine labda ile harufu inaweza kutoka humo, lakini hakukuwa na dalili yoyote.




Alipohakikisha kuwa mle ndani hakuna kitu. Akalifunga, lakini tayari alishaanza kukohoa na kupiga chafya. Mafua kwa mbali yalionekana kumuanza, kwani alihisi kama pia moja inaziba.

Akazunguka pembe zile nne cha chumba kuangalia, lakini wapi. Akaamua kuchukua fagio. Akalala kifudifudi na kuupitisha ufagio uvunguni kwa kitanda ili kuona kama anaweza kufanikiwa.

**Akazunguka pembe zile nne cha chumba kuangalia, lakini wapi. Akaamua kuchukua fagio. Akalala kifudifudi na kuupitisha ufagio uvunguni kwa kitanda ili kuona kama anaweza kufanikiwa.**

Alipokuwa akipeleka fagio ndani, akavuta kwa nje, kuona nini kitatoka.

Mara ya kwanza ilitokea leso ambayo tayari ilikuwa imechakaa. Nadhani ilikuwa ni moja kati ya leso zake zilizopotea bila kujua zimekwenda wapi.

"Hawa hawa panya wanazibeba." Akajiambia mwenyewe.

Akafanya kama mwanzo, safari hii kuna kitu kigumu ambacho kilikuwa kinalia kwa sababu ya msuguano wake na sakafu chini.

Kilichotokea na kukiona machoni mwaka ni sarafu mbili za shilingi mia tano. "Hizi ndiyo zile ambazo huwa zinaanguka kwenye mfuko wa shati, halafu zinaingia uvunguni." Akaongea kwa sauti kama vile anamwambia mtu.

Alipoipata ile buku kwanza alisimamisha zoezi. akazichukua na kwenda kuziweka juu ya meza.

Kazi ya kumtafuta panya ikaendelea. Kwa sababu tayari alishamaliza chumba kizima kama yeye alivyodhani, basi sehemu ya mwisho ilikuwa ni chini ya uvungu wa kitanda.

Kama angekuwa na nguvu angeweza kukinyanyua kitanda na akapata nafasi ya kuangalia kililichomo chini ya uvungu, lakini kitanda chake jinsi kilivyo hata watu wawili wangeweza kunyanyua kwa shida sana.

Kitu ambacho hata hao watu wawili wangeweza kufanya ni kufungua nati zilizounga mbao za kitanda hicho, halafu ndiyo wasaidiane kunyanyua vipande vyake na chaga, wakishamaliza wafunge tena nati, warejeshe chaga ili kirudi kwenye hali yake ya kawaida. Lakini wapi.

Pamoja na kwamba feni ya kusimama ilikuwa inampepea, lakini jasho lilikuwa linammimikika.

Alifanya tena kama mwanzo, lakini safari hii alisogea pembeni kidogo, ili aone nako anatoa nini.

Safari hii ufagio ulikuwa mgumu kidogo na sauti ya kukwaruza ikasikika. "Haa, kumbe ni chupa ya soda!" Akashangaa na kukasirika kwa wakati mmoja.

Alichoona ni kwamba zoezi lake kama linakwenda kufeli, kwani muda nao ndiyo unakaribia.

Kwa bahati mbaya sana mpenzi wake huyo mpya, Nuru hakuwa na simu ya mkononi. Au alikuwa nayo, lakini alidanganywa na hakupewa namba.

Kama angekuwa na namba angeweza kumpigia na kumwambia leo asiende kwa sababu ametoka nyumbani mpaka Jumapili ijayo.

Walivyokubaliana na kwamba akifika eneo ambalo alimwambia kuna kibanda kinachouzwa juisi ya miwa, mbele yake atakuta mlango ambao hufungwa muda wote, lakini siyo na komeo hadi saa tatu usiku, hivyo asukume mlango na kama akikuta kuna watu uani, basi amuulize kwa jina hilo hilo la Heri.

Na kama hakukuwa na watu, basi akamwambia chumba chake ni cha upande wa kulia, akiingia kwenye mlango huo mkubwa ambao wao waliufanya kama 'geti', ukiingia tu unatokea kwenye ua unaotenganisha mabanda ya uani na nyumba kubwa.

Pia alidhani angekuwa na simu wangeweza kuwa hata wanawasiliana kujua yupo wapi saa hizi hata kama anakuja, lakini kwa sasa anachosubiri ni kugongewa hodi tu. Na hicho ndicho kilichomtia presha zaidi.

Heri akasogea pembeni tena ya kitanda na kujaribu kukokota kile ambacho kipo uvunguni, na lengo ni kumtoa panya aliyekufa ambaye anatoa harufu kali.

Kilichotoka sasa ni mtego wa panya. Lakini haukuwa mzima. Ulikuwa ni mtego wa zamani ambao uliharibika. Tangu uharibike hajanunua mtego mwingine. Ulikuwa umeshaanza kuwa na kutu, ukiwa hauna uwezo wa kukamata hata mende, achilia mbali panya, kwa sababu waya na vitu vingine ambayo vinasababisha uitwe mtego vimeshaharibika.

Hapo akachoka zaidi. Akaachana na alichokuwa anafanya, akakaa chini.

Dakika mbili baadaye akasimama na kuzunguka chumba kizima, akitafuta kitu kile kile na sehemu zile zile ambazo ameshapita. Hakuna kilichobadilika.

Alipoangalia saa yake kwenye simu yake ya kitochi ilimwambia imebaki nusu saa tu mgeni awasili.

Wakati wenzake wanakuwa na furaha wanapokuwa na ahadi na wapenzi wao, yeye sasa alichukia.

Akatamani Nuru apate dharula yoyote ile asifike siku hiyo. Harufu iliendelea kuzidi na kuanza kumsumbua hata yeye mwenyewe. Akakaa kwenye kitanda kwanza ili atulize akili na kuona nini cha kufanya.

Mawazo yakamrudisha nyuma, siku ya kwanza alipokutana na Nuru.

ITAENDELEA JUMAPILI



# YAKOBO MWAMBOYA MBONA AMEKUELEWA

MWIMBAJI wa muziki wa Injili anayetikisa jiji la Mbeya, Yakobo Mwamboya, amesema anawashukuru Watanzania kwa kumpatia nguvu ambayo inamfanya kutunga nyimbo zinazokubaliwa na watu wengi bila kujali imani yake.

Akizungumzia mafanikio aliyoyapata baada ya kutambulisha wimbo wake mpya 'Nimekuelewa' amesema kutokana na nguvu za nyimbo zake, idadi kubwa ya watu wanamtafuta na kumpongeza kutokana na kipaji kikubwa alichonacho.

"Mapokezi yamewkuwa makubwa, Mungu ametusaidia kutoa wimbo huu ambao kwangu ni ushuhuda na ninashukuru umeweza kuwagusa wengi ambao wametendewa mambo makubwa na Mungu, naomba mashabiki waendelee kuniunga mkono ili nifike mbali," amesema Mwamboya.



# JERRY A MWENDO WA MATEKA

Msanii wa Bongo Fleva, Jerry A, ameendelea kukonga mioyo ya mashabiki wake baada ya kuachia wimbo wake mpya 'Mateka' ambao umepokelewa vizuri.

Mwanamuziki huyo aliyejikita katika nyimbo za mahaba, ameliambia Nipashe kwamba wimbo huo ni maalumu katika msimu huu wa sikukuu ameuachia juzi kwa njia ya audio na video yake itatoka hivi karibuni.

"Nimeendelea kuwapa burudani mfululizo mashabiki zangu na safari hii nimewaletea ngoma hii, Mateka ambayo imebeba hisia tofauti kwa mashabiki zangu, video nitaitoka katika sikukuu ya Ramadhani hivyo mashabiki wake tayari," amesema Jerry A.

## ZISIKUPITE

### PSG YAMTAKA OSIMHEN
KLABU ya Paris St-Germain ipo tayari kulipa pauni milioni 111.5 ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Napoli msimu huu. **(Corriere dello Sport**)

### DOVBYK ANUKIA CHELSEA
CHELSEA inaendelea kutafuta mshambuliaji mbadala wa Victor Osimhen, huku mchezaji wa kimataifa wa Ukraine na Girona, Artem Dovbyk, mwenye umri wa miaka 26 akiwa kwenye rada za klabu hiyo. (**GiveMeSport**)

### TEN HAG KUBAKIA UNITED
MANCHESTER United inapanga kumtumia Erik ten Hag kama kocha muda wa klabu hiyo kutokana na kukosekana kwa mbadala wake. (**i news**)

### SAVIO AKARIBIA CITY
KLABU ya Manchester City imekubali dili la kumsajili winga wa Troyes, Mbrazil Savio mwenye umri wa miaka 19, ambaye yuko Girona kwa mkopo. (**Football Insider**)

### SANCHO MAMBO BADO
MAHITAJI ya Manchester United ya kutaka ada ya pauni milioni 34 kwa ajili ya Jadon Sancho yanaweza kukatiza nia ya winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 24 kutaka kurejea kwa mkopo Borussia Dortmund ili kuwa wa kudumu. (**Sky Sport**)

### AMORIM NJIA PANDA
KOCHA wa Sporting Lisbon anayenyatiwa na Liverpool Mreno Ruben Amorim mwenye umri wa miaka 39, amekiri "hawezi kukuthibitisha" kama atakuwa mwalimu wa klabu hiyo ya England katika msimu ujao. (**ESPN**)

### JAMES YUKO SOKONI
CHELSEA haitazingatia ofa za kumnunua beki wa England, Reece James, mwenye umri wa miaka 24, msimu huu licha ya tetesi zinazomhusisha mchezaji kutakiwa na PSG au Real Madrid. (**Football Insider**)

### NEWCASTLE: BRUNO HAONDOKI
KOCHA Eddie Howe ameelezea azma yake ya kumbakisha Bruno Guimaraes katika kikosi cha Newcastle United, huku Magpies hao wakijiandaa kuzuia klabu nyingine kumnunua kiungo huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 26. (**Mirror**)


### CITY KUMUUZA PHILLIPS
KLABU ya Manchester City iko tayari kupata hasara kubwa kwa kumuuza kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 28 msimu huu. (**Football Insider)**

### DEWSBURRY KUTUA SPURS
TOTTENHAM Hotspur inapania kumnunua kiungo wa Leicester City, Kiernan Dewsbury-Hall mwenye umri wa miaka 25, ambaye anaweza kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 25 klabu yake itashindwa kupanda daraja kurejea Ligi Kuu England. (**Talksport**)

### FATI AGOMBEWA ULAYA
MSHAMBULIAJI asiyetakikana wa Barcelona, Ansu Fati, mwenye umri wa miaka 21, hatarejea Brighton msimu ujao - lakini Wolves, Sevilla na Valencia zote zinafikiria kumnunua nyota huyo wa Hispania kwa mkopo. (**Sport**)

### BURNLEY KUMSAJILI SAMBO
KLABU ya Burnley imekubali kumsajili beki wa Uholanzi, Shurandy Sambo, msimu wa joto mara baada ya mkataba wa mchezaji huyo wa PSV Eindhoven kumalizika. (Fabrizio Romano)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# ZINCHENKO: NINAWEZA KWENDA VITANI UKRAINE

**Beki huyo wa Arsenal asema yuko tayari kuiacha klabu kwa ajili...**

**LONDON,** England

MLINZI wa pembeni wa Arsenal, Oleksandr Zinchenko, amesema atarejea Ukraine kupigana katika vita kwa ajili kulilinda taifa lake iwapo ataitwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 tayari ametoa pauni milioni moja kusaidia wale waliorejea nyumbani baada ya uvamizi wa Urusi nchini Ukraine tangu mwaka 2022.

**Alipoulizwa na Newsnight ya BBC kama atajibu simu akiitwa, Zinchenko alisema: "Nadhani ni jibu la wazi. Nitaenda."**

Alisema marafiki zake kadhaa wa zamani wa shule tayari wamejiunga na Jeshi la Ukraine.

"Ni vigumu kuelewa hivi majuzi tu tumekuwa katika shule moja, tulikuwa tunacheza kwenye uwanja wa michezo au kwenye uwanja wa mpira wa miguu, na sasa wanapaswa kulinda nchi yetu," alisema.

"Kusema kweli, ni vigumu sana kukubali hili, lakini ndivyo lilivyo. Hatuwezi kukata tamaa."

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, wiki hii alitia saini muswada wa kupunguza umri wa uhamasishaji wa kujiunga na jeshi kutoka miaka 27 hadi 25.

Zinchenko alianza maisha yake ya soka nchini Urusi akiwa na Ufa kabla ya kujiunga na Manchester City mwaka 2016 ambapo alishinda mataji manne ya Ligi Kuu England.

Alihamia Arsenal Julai mwaka, 2022 kwa ada ya pauni milioni 35.

Aliongeza hana mawasiliano kidogo na wachezaji wenzake wa zamani wa Urusi.

"Tangu uvamizi huo ni wachache sana wamenitumia meseji na siwezi kuwalaumu kwa sababu hili si kosa lao," alisema.

"Siwezi kuwaambia, 'jamani, fanyeni maandamano kupinga haya yote', kwa sababu najua wanaweza kufungwa gerezani."



# ANGE: SPURS HAINA WASIWASI NA USAJILI

**LONDON,** England

ANGE Postecoglou amesisitiza hasara ya karibuni ya Tottenham Hotspur ya pauni milioni 86.8 haitaathiri mipango ya uhamisho wa klabu hiyo majira ya joto na anaamini bado wako katika nafasi nzuri zaidi ya kutumia kuliko wapinzani wao wengi kwenye Ligi Kuu England.

Spurs mapema wiki hii walichapisha matokeo yao ya hivi punde ya kifedha kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2023, ambayo yalikuwa na upungufu mkubwa licha ya mauzo kuzidi pauni milioni 500 kwa mara ya kwanza.

Vyanzo vimeiambia ESPN, Tottenham bado wana nafasi muhimu katika kufuata Kanuni za Faida na Uendelevu za Ligi Kuu, tofauti na klabu nyingine kadhaa ikiwa ni pamoja na Nottingham Forest na Everton, ambao tayari wamekatwa pointi msimu huu kwa uvunjaji wa kanuni za fedha.

"Majadiliano yangu kuhusu aina hizo za masuala ni tofauti," alisema Postecoglou.

"Sio kama 'oh tutasubiri matokeo ya kifedha kabla ya kuanza kufikiria ni nani tutamsaini.' Mambo haya yote tayari yanapangwa. Tunajua tuko katika nafasi gani na tunahitaji kufanya nini wakati wa kiangazi.

"Hiyo haimaanishi kuwa yote yatatimia bila shaka kwa sababu kuna kila aina ya mambo mengine ambayo yanakuja. Lakini mipango yetu inaendelea vizuri katika kile tunachohitaji kufanya.

"Hakuna shaka kwa mtazamo wetu, sisi sio moja ya klabu ambazo zitawekewa vikwazo."

Postecoglou amedai mara kwa mara mabadiliko ya timu yake ni muhimu zaidi kuliko kufuzu tu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya na aliitaja Newcastle United kama mfano wa timu iliyocheza katika mashindano ya msimu huu, lakini imeshuka kwa ujumla kwa sababu ilitolewa katika hatua ya makundi na ipo nafasi ya nane kwenye jedwali la Ligi Kuu England.

# Pochettino alia na mashabiki Chelsea

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amekabiliwa na vita kali akijaribu kuwashinda mashabiki waaminifu wa Chelsea tangu alipoweka kalamu kwenye mkataba wa miaka miwili ya kuhudumu hapo Stamford Bridge.

Kocha huyo raia wa Argentina amebainisha itakuwa ngumu kwa Chelsea kumpata kocha mvumulivu wa mashabiki kwa kuzomewa kama yeye.

"Wanapopata ushindi wapo pamoja na mimi, tukishindwa, wananiona tena mimi sifai," alisema Pochettino.

Alifika kwenye klabu kama gwiji wa Tottenham Hotspur, mbunifu nyuma ya moja ya vipindi vya kukumbukwa zaidi katika historia yao.

Mashabiki wa London Kaskazini hata waliimba jina lake kwa matumaini ya kumrejesha miezi kadhaa kabla ya kusajiliwa na The Blues.

Raia huyo wa Argentina hajarahisisha maisha yake kutokana na baadhi ya matendo kufikia sasa katika kipindi chake kifupi.

Kabla ya mkutano wa Novemba na Spurs, alifanya kidogo kuonyesha uaminifu usioisha kwa klabu yake ya sasa.

"Ni muhimu sana kurudi kwa sababu baada ya miaka minne mahali tuna kumbukumbu za kushangaza na kuunda kumbukumbu za kushangaza pamoja, nadhani ni maalum. Siwezi kusema uongo," alisema Pochettino wakati huo, kabla ya kukiri hakuhisi upendo wa aina moja kwa mashabiki wa Chelsea.

Stamford Bridge pamekuwa mahali pa hasira na uasi, ambayo inaeleweka kutokana na takriban miongo miwili ya mafanikio ambayo yalitangulia kabla ya ujio wa BlueCo chini ya Todd Boehly.



## Amorim sasa aivuruga Liverpool

**LIVERPOOL,** England



KOCHA wa Sporting CP, Ruben Amorim, ameiweka Liverpool katika hali ya tahadhari na kukiri, tofauti na Xabi Alonso, yeye hawezi kusema kwa uhakika kama hatabadilisha klabu msimu huu wa joto.

Liverpool walikuwa wakimwinda Alonso kabla ya kuthibitisha hadharani uamuzi wake wa kusalia Bayer Leverkusen hadi mwisho wa msimu huu, na kuwapa pigo kubwa Wekundu hao na Bayern Munich katika mchakato huo.

Amorim tangu wakati huo ameibuka kama mgombeaji mkuu wa kuchukua mikoba ya Jurgen Klopp na kocha huyo mwenye umri wa miaka 39 alichochea uvumi huo kwa kukataa kuondoka uwezekano wa kujiunga na simu mpya msimu wa joto.

Alipoulizwa kama anaweza kuhakikisha kubaki na Sporting, Amorim alisema kwa uwazi: "Hapana, siwezi kukuhakikishia."

Aliendelea: "Michezo tayari inashughulika na siku zijazo, siwezi kuamua. Nilitoa neno langu na siwezi kurudi nyuma.

"Kama hatutashinda mataji nitaondoka Sporting, ilikuwa wazi tangu mwanzo ni dau nililopeleka kwa wachezaji, lazima tushinde mataji, kwanza tuone kama tunaweza kufanya hivyo. Nitaamua mambo.

"Sio wasiwasi, siku zijazo zimepangwa kwa muda mrefu. Tunaelezea hali zote za msimu ujao. Kwa hivyo siwezi kukuhakikishia kuwa nitabaki, lazima tushinde mataji. Na tuko kwenye mbio, tupo njia sahihi."

Mkataba wa Amorim na Sporting una kipengele cha kutolewa ambacho ripoti zinaonesha kuwa ni kati ya pauni milioni 10 na milioni 15.

Iwapo Liverpool, au upande wowote, utaanzisha kifungu hicho, Sporting haitakuwa na uwezo wa kumzuia Amorim.

HABARI MICHEZO

# MSHAMBULIAJI WA KMC BADO AITAMANI YANGA

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI wa KMC FC, Waziri Junior, ambaye aliwahi kuichezea Yanga, amesema iwapo angepewa muda na kuvumiliwa, basi saa hizi klabu hiyo ingekuwa inakula matunda yake kwa kuwafungia 'mabao muhimu' katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Waziri Jr amefunga mabao 11 mpaka sasa akiwa katika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora nyuma ya Stephane Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC wenye mabao 13 kila mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Waziri Jr, alisema kama aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, angebaki katika kikosi hicho, anaamini angepata nafasi ya kufanya makubwa na anadhani angekuwepo hadi leo hii.

Nyota huyo amepinga mawazo ya baadhi ya mashabiki wanaodai yeye ni mchezaji wa daraja la kati tu na si la juu, hivyo hawezi kung'ara katika klabu kubwa, badala yake ataendelea kuwika kwenye klabu ndogo kama KMC anayochezea sasa. "Unasajili mchezaji humpi nafasi ya kucheza, au unampa mechi chache utasema huyo mchezaji ni wa daraja la kati? Kocha, Cadric Kaze alinipa nafasi katika mechi tatu nikafunga goli moja," alisema straika huyo.

Alimsifu pia Nabi kuwa ndiye kocha aliyempa nafasi na kumfanya awe bora, na hata alipotoka, mazoezi yake yamemfanya awe mchezaji mzuri akiwa KMC.

"Nabi ndiyo mtu aliyenipa nafasi mpaka msimu unaisha, mwalimu ndiyo atamfanya mchezaji awe bora, angebaki ningefanya makubwa ndani ya Yanga," Waziri Jr alisema.

Mchezaji huyo ambaye pia ameshawahi kuicheza Azam FC, aliondoka Yanga mwaka 2021, na alitua Jangwani akitokea Mbao FC ya jijini, Mwanza.



Wachezaji chipukizi kutoka sehemu mbalimbali jijini, Dar es Salaam wakifanya mazoezi ili kuboresha vipaji vyao kwenye viwanja vya JKM Park jana asubuhi. PICHA: JUMANNE JUMA

# Ifakara Queens yaichapa Kilosa

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

TIMU ya Ifakara Home Queens imeendelea kutoa dozi baada ya kuifunga Kilosa Queens mabao 3-0 katika mechi ya Ligi ya Wanawake ya Mkoa wa Morogoro iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa jana.

Kwa ushindi huo, Ifakara Home Queens inashika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inayosimamiwa na Chama Cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Morogoro (MWFA), G-Seven ndio vinara.

Mabao ya Ifakara Queens katika mchezo huo yalifungwa na Monica Mwasakilale, Rahel Jonas na Veronica Hangahanga.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa jana, G- Seven ilipata ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Ulanga Queens.

Naye Mwenyekiti wa MWFA, Beatrice Selemani, alisema msimu huu ligi hiyo imekuwa na ushindani kutokana na maandalizi mazuri ambayo timu zote wamefanya.

Mwenyekiti huyo alisema anazipongeza timu zote kwa ushiriki wao na anaamini bingwa atakayepatikana ataenda kuiwakilisha vyema Morogoro katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa wa Mikoa kwa Wanawake yatakayofanyika baadaye mwaka huu.

"Vifaa vimekuwa ni changamoto kwa wachezaji, tunaomba wadau waliangalie kwa jicho la huruma ili tusaidie kukuza vipaji vya wachezaji wetu wanawake," alisema kiongozi huyo.

## Azam FC, Mtibwa hapatoshi FA Cup

INATOKA UK. 24

Dabo alisema hawatawadharau wapinzani wao kwa sababu anafahamu leo wataingia na mbinu tofauti baada ya kujiimarisha kwa kufanyia kazi mapungufu yao.

"Tunaenda katika mchezo wa mtoano ambao kila timu inahitaji kutafuta ushindi kwa ajili ya kusonga mbele, tutapambana ili kupata ushindi, tuko tayari kwa mechi hii," alisema Dabo.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema akiandaa vizuri kikosi chake na anataka kutumia mashindano hayo kuwafurahisha mashabiki wao kutokana na kutofanya vyema katika michezo ya Ligi Kuu msimu huu.

Katwila alisema anatambua ubora wa Azam na ili kuvuna matokaeo chanya, amewaandaa wachezaji wake kupambana na kuhakikisha wanaiondoa Azam katika michuano hiyo.

"Hakuna mechi rahisi katika mashindano haya ya mtoano, timu zote zilizofika hatua hii ni bora, na kila mmoja anatamani kuona atafuzu hatua ya robo fainali, tutaenda kupambana kwa wakati wote," Katwila alisema.

Aliongeza kwa kuwataka washambuliaji wake kuongeza utulivu huku mabeki kuimarisha safu yao ili kutoruhusu wenyeji kutawala mchezo huo.

## Yanga yamshtaki Rasmi mwamuzi

INATOKA UK. 24

kushindwa kuzitumia, tumecheza vizuri, ila hahitaji hata msaada wa VAR kujua kama lilikuwa bao au la, tulistahili kupewa, nimesikitishwa na maamuzi ya waamuzi wa mchezo.

Mwamuzi hataki kuangalia VAR? Labda kuogopa watu wakubwa. Tunarejea nyumbani kujiandaa na michezo iliyopo mbele yetu," alisema Gamondi.

"Mchezo mzuri Yanga. Mmeonyesha kiu na juhudi ya kuiletea heshima nchi yetu hadi kufikia hatua hii. Tunatarajia makubwa zaidi kutoka kwenu kwenye mashindano haya ya Ligi ya Mabingwa ya Shirikisho la Soka Afrika msimu ujao. Tutaendelea kuwaunga mkono na kuwapa motisha," aliandika Rais Samia.

Kipa wa Mamelodi Sundwons, Ronwen Williams, ambaye aliokoa penalti nne katika mechi moja ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) mapema mwaka huu akiwa na Afrika Kusini, aliibuka tena shujaa kwa kuokoa penalti mbili zilizopigwa na Aziz Ki na Dickson Job, huku ile ya Ibrahim Hamad 'Bacca', ikipaa.

Waliofunga penalti za Yanga ni Augustine Okra na Joseph Guede.

Penalti za Mamelodi ziliwekwa wavuni na Marcelo Allende, Lucas Ribeiro, Neo Maema, huku kipa wa Yanga, Djigui Diarra akipangua penalti ya Leandro Siniro.

Kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Cairo, Misri, Simba iliondolewa katika michuano hiyo baada ya kufungwa mabao 2-0 na mabingwa watetezi, Al Ahly.

Mabao ya Al Ahly katika mechi hiyo iliyowafanya wasonge mbele kwa ushindi wa jumla wa magoli 3-0 yaliwekwa wavuni na Amr El Solia na Mahmoud Karhaba.

Baada ya mechi hiyo iliyochezwa kuanzia saa 5:00 usiku, Rais Samia pia akawafariji akiandika tena kwenye akaunti yake ya instagram.

"Mchezo mzuri Simba. Usiku haukuwa wa ushindi lakini tumeziona juhudi na zinatupa faraja na matarajio kuwa, msimu ujao wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa ya Shirikisho la Soka Afrika mambo yatakuwa mazuri zaidi. Ahadi yetu ni kuendelea kuwaunga mkono na kuwapa motisha." Yalikuwa ni maneno ya kuwatia moyo wawakilishi hao ambao ni mara ya pili mfululizo wakitolewa hatua hiyo, msimu uliopita wakitolewa dhidi ya Wydad Casablanca kwa penalti 4-3.

Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, alisema hakuna wa kulaumiwa katika hilo kwa sababu wachezaji wake wamepambana kwa uwezo wao wote, lakini wameshindwa kupata mabao na Al Ahly licha ya kucheza nyumbani, lakini walipaki basi na kushambulia mara chache, hatimaye wakapata walichokihitaji.

"Tumepambana, lakini hatukufanikiwa, hii ni timu kubwa sana Afrika, inahitaji zaidi ya hiki tulichonacho, hakuna wa kulaumiwa, nadhani msimu ujao tutarudi tukiwa imara zaidi ya hivi," alisema kocha huyo.

Timu hizo sasa zinarejea nchini kuendelea na mechi zao za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA.

# Michezo

Jumapili Aprili 7, 2024

Nipashe




## Pochettino alia na mashabiki Chelsea

UKURASA 22





Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza (picha kushoto-jezi ya bluu), akiruka juu kuwania mpira dhidi ya nyota wa Al Ahly ya Misri. Kulia mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki, akipambana kumtoka mchezaji wa Mamelodi Sundowns katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa jijini, Pretparia jana usiku. **PICHA: MITANDAO**

# YANGA YAMSHTAKI RASMI MWAMUZI CAF

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### Rais Samia awafariji Simba, Yanga, makocha wakiri wamecheza dhidi...

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan akituma salamu za faraja kwa Simba na Yanga baada ya kuondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa Yanga umewasilisha rasmi malalamiko yake katika Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kuhusiana na maamuzi ya mchezo wao uliochezwa kwenye Uwanja wa Tshwane-Loftus Versfeld jijini Pretoria, Afrika Kusini.

**Yanga imeondolewa katika michuano hiyo kwa penalti 3-2 na wenyeji, Mamelodi Sundowns wakati Simba iliaga michuano hiyo kwa kukubali kufungwa magoli 2-0 na Al Ahly ya Misri.**

Katika malalamiko yao, Yanga inadai ilifunga bao halali dakika ya 57 kupitia mchezaji wake, Aziz Ki Stephane (aliyevaa jezi namba 10), lakini likakataliwa na waamuzi waliochezesha mechi hiyo wakiongozwa na Dahane Beida kutoka Mauritania.

Yanga inadai Beida na wasaidizi wake waliokuwa katika VAR, Daniel Ayi kutoka Ghana na Jerson Dos Santos wa Angola, kwa sababu zao walikataa kupitia marejeo na kwa kufanya hivyo walikiuka kanuni za matumizi ya teknolojia hiyo jambo ambalo halikuwa sahihi na haki kwenye mpira wa miguu.

Yanga pia inadai matukio mbalimbali yaliyokuwa yanafanywa na mwamuzi huyo wa kati yalikuwa na viashiria vya upangaji matokeo katika mchezo huo wa robo fainali ikiwamo kutotoa adhabu ya kadi nyekundu kufuatia faulo aliyofanyiwa mchezaji wake akiwa anaelekea kufunga.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara pia wanalalamikia hakukuwa na haki kwenye uamuzi na kutilia shaka weledi wa mwamuzi huyo wa Mauritania.

Yanga inaiomba CAF kufanya uchunguzi kutokana na matukio mbalimbali ili kubaini yalifanyika kwa makosa ya kibinadamu au yalilenga upangaji wa matokeo.

Yanga imeweka wazi imelazimika kuwasilisha malalamiko yake kwa kufuatia Kanuni ya 16 (3) ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ya CAF.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ametupa lawama zake kwa Beida akidai aliwapendelea wenyeji.

Gamondi alisema ni mbeleko ya chuma ndiyo iliyowapeleka Mamelodi Sundowns hatua ya nusu fainali na si vinginevyo.

"Tumecheza na timu kubwa, vijana wamepambana, tumetengeneza nafasi na

INAENDELEA UK 23

## Azam FC, Mtibwa hapatoshi FA Cup

**Na Saada Akida**

AZAM FC inatarajia kuikaribisha Mtibwa Sugar katika mechi ya hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Kombe la CRBD Bank FA itakayochezwa leo kuanzia saa 3:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Timu hizo zinakutana kwa mara ya tatu katika msimu huu, mara mbili katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo zote Azam iliondoka na ushindi.

Tayari Namungo FC, Geita Gold FC, Tabora United na Coastal Union zimeshatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema timu yake imejiandaa vyema kuelekea mchezo huo na anaamini hautakuwa rahisi licha ya kuwafunga Mtibwa kwenye michezo yote ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >